

**EU** yaipatia Tanzania bil. 97/- kusaidia bajeti 2024/25

UKURASA 2



**Wadau** waomba kuondolewa VAT vifaa nishati safi

UKURASA 4



**Wenje** ajitosa kinyang'anyiro Makamu M/Kiti wa CHADEMA

UKURASA 10

**PSG YAMTWAA NEVES KUTOKA BENFICA**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Agosti 7, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581761

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US www.twitter.com/nipashetz

www.ippmedia.com www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Kupiga 'chabo' tatizo la akili

• **Mwanasaikolojia** abainisha kwa kina, wanaojifungua wapaza sauti ...

*Endelea ukurasa 7*



## Tanzania sasa namba 2 uzalishaji wa tumbaku UK. 2



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akikagua moja ya maabara ya afya ya mimea, baada ya kuzindua jengo mtambuka la mafunzo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kampasi ya Edward Moringe, mkoani Morogoro jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 5

### TAKUKURU YARIDHISHWA NA UJENZI BARABARA

KAMANDA wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma, Hamza Mwenda, amepongeza Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) mkoani humo kwa kufanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ...

UKURASA WA 20

### UWANJA KUCHEZA LIGI KUU NI KUANZIA WATAZAMAJI 3,000

MADAI BINTI KUBAKWA

## Watuhumiwa mikononi mwa dola, makundi zaidi yajitokeza kulaani

UKURASA 3

**MICHEZO** **HOMA YA DABI SIMBA, YANGA NYUZI JOTO 90** UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA




Balozi mpya wa India nchini, Bishwadip Dey, akiwasilisha hati za utambulisho kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania sasa namba 2 uzalishaji tumbaku

**Christina Haule na Idda Mushi, MOROGORO**

TANZANIA ni mzalishaji namba mbili wa tumbaku duniani baada ya Zimbabwe, hatua iliyofikiwa baada ya uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kubadilisha sera na kuvutia uwekezaji uliowezesha wakulima kupata pembejeo.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo wakati akimkaribisha Rais Samia kufungua Kiwanda cha Mkwawa Leaf Serengeti, wakati wa ziara ya kikazi mkoani humo kukagua miradi ya maendeleo na kuzungumza na wananchi.

"Baada ya kukamilika kwa upanuzi kinakuwa kiwanda cha pili duniani kwa uchakataji wa tumbaku, hatua ambayo itawaongezea kipato wakulima kwa kuwa watakamilisha hatua zote kupata bidhaa nchini," alisema Bashe.

Alisema uwekezaji uliofanyika kwenye kiwanda hicho ndio maana halisi ya ziara za Rais Samia nje ya nchi na kufanya mabadiliko ya kuvutia wawekezaji iliyowezesha wakulima kupata pembejeo na mazingira mazuri ya kufanyakazi zao.

Alisema matokeo ya uamuzi wa Rais Samia kuhusu Kiwanda cha Tumbaku mkoani Morogoro ndio umeleta matokea chanya kwa upanuzi huo kukamilika na wakulima kuwa na soko la uhakika.

"Wakati anachukua uongozi, uzalishaji wa tumbaku ulikuwa tani 65,000. Kwenye sekta ya tumbaku pia kuna kitu kinaitwa makinikia kama ilivyokuwa kwenye dhahabu. Makinikia wanunuzi walikuwa wanaingia mkataba na wakulima, wanampa mbegu na kutaka wazalishe kilo 1,000," alisema.

"Mkulima anabaki na tumbaku, kama bei ni dola moja, wanampa 0.5. Kwa hiyo mheshimiwa Rais leo Tanzania inashika nafasi ya pili kwa uzalishaji wa tumbaku Afrika baada ya Zimbabwe.

Bashe alisema ni zaidi ya Dola milioni 400 kwa usafirishaji wa zao la tumbaku, kwa msimu Tanzania iliweka lengo la kuzalisha tani 170,000 hadi 200,000, lakini wamezalisha tani 122,000.

Kwa mujibu wa Waziri Bashe, tumbaku imeongezeka kutoka wastani wa Dola 1.4 mpaka 2.4 na kuchakata tani 80,000 na kwamba maboresho hayo zitachakatwa tani 200,000.

**ELIMU**

Akizindua jengo mtambuka la mafunzo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA, lililoitwa Dk. Samia Suluhu Hassan Teaching Complex, alivitaka vyuo vikuu nchini kuendelea kufanya utafiti unaotoa majibu kwenye mahitaji ya jamii na kimataifa badala ya kuishia kwenye vitabu na majarida ama mashindano ya tuzo.

Akizindua jengo hilo la maabara jumuishi au mtambuka lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,205 kwa wakati mmoja, aliwapongeza SUA kwa kujiongeza na kutoa fedha za ndani kiasi cha Sh. bilioni 2.6 kukamilisha jengo hilo ambalo serikali ilitoka Shilingi bilioni tisa.

"Nilipoingia ndani nimekuta wanafunzi kutoka nchi za Afrika Mashariki, Magharibi na Kusini, zamani sisi ndio tulikwenda kujifunza huko, lakini sasa na wao wanakuja, ni fahari kubwa kwa nchi yetu," alisema.

**KULINDA AMANI**

Rais Samia aliwataka Watanzania kutambua kuwa suala la ulinzi na usalama ni la wote bila kujali sehemu au sekta mtu anayofanyia kazi na hawatakiwi kupuuzia dalili zozote zinazoweza kuhatarisha amani ya nchi kwa kuwa njiti moja ya kibiriti inaweza kuchoma msitu mzima.

Akizungumza na wananchi mjini Morogoro katika Uwanja wa Jamhuri, alisema kampeni ya TUTUNZANE aliyoizindua inalenga kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji kwa kuhamasisha na kuwezesha ufugaji na kilimo cha kisasa na kila mmoja anapaswa kuwa na eneo lake la kilimo ua malisho.

Aliwataka wakulima na wafugaji wafanye kazi kwa pamoja, wategemeane na wasivunjwe moyo wa kutekeleza kampeni hiyo.

**UPANUZI HOSPITALI**

Alisema Shilingi bilioni tano zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa Hospitali ya Rufani mkoani Morogoro ili kukidhi mahitaji ya kutoa huduma kwa jamii kutokana na iliyopo kuzidiwa na wagonjwa.

Samia alisema fedha hizo zitakazotokana serikalini zilitengwa katika kipindi cha mwaka 2021/24 kukamilisha vituo 136 vya afya ili kuimarisha huduma za mama na mtoto.

**VIWANDA**

Rais Samia alisema ufufuaji wa viwanda utaanza kwa kukifufua kiwanda cha vipuli kilichoko Mang'ula wilayani Kilombero na kuhakikisha vilivyopo havifi bali vinafufuliwa kikiwamo cha mafuta ya alizeti ili kuwapo kwa ajira kwa vijana na kukuza uchumi wa mkoa.

Alisema historia ya Morogoro ina nafasi ya viwanda uwekezaji mpya na upanuzi wa viwanda mkoani hapa ni ishara ya uzuri wa sera za uwekezaji na ishara kwamba wakulima ni wazalishaji wazuri.

Pia, aliwataka wazazi kuwapeleka vijana wao kupata elimu kwenye vyuo vya ufundi (VETA) vilivyopo nchini ili kunufaika kwa kupata ajira kupitia viwanda vinavyoanzishwa.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, alisema wakati kiongozi huyo anaingia madarakani alikuta viwanda 62,000 na kufanikiwa kuviongoza kufikia 80,000.

"Hili ni ongezeko la viwanda 18,000. Kiwanda hiki kitaajiri zaidi ya watu 7,000, Mkoa wa Morogoro pekee kuna viwanda 3,247 vilivyoajiri zaidi ya watu 51,426. Rais Samia anahakikisha sekta ya viwanda inafanya vizuri," alisema.

Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, aliishukuru serikali kwa kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo nchini sambamba na kutenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Mabasi Msamvu.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, aliishukuru serikali kwa kuwapatia miradi sekta mbalimbali yenye thamani ya Sh. bilioni 343.3 ikiwamo elimu, afya na miundombinu.

Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdul Aziz Abood, aliiomba serikali kujenga hospitali nyingine ya rufani mkoani hapa ili kutoa huduma sambamba na iliyopo na kukidhi utoaji wa huduma kutokana na hospitali iliyopo kuzidiwa na wagonjwa.

Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Hamisi TaleTale, aliiomba serikali kuona umuhimu wa kukipa hadhi kwa kuboresha majengo na huduma kwenye kituo cha afya Ngerengere kinachokabiliwa na ukosefu wa huduma muhimu ikiwamo chumba cha kuhifadhia maiti.

## EU yaipatia Tanzania bil. 97/- kusaidia bajeti

**Na Christina Mwakangale**

UMOJA wa Ulaya (EU), umeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 33.12 (sawa na Sh. bilioni 97) kwa ajili ya kusaidia mageuzi ya kisekta yanayoendelea nchini.

Fedha hizo zimegawanywa katika sekta tano muhimu, zinazolenga kukuza maendeleo kijamii, kiuchumi na kuongeza ustahimilivu wa wananchi wa Tanzania.

Balozi wa EU nchini, Christine Grau, alisema haya jana katika taarifa kwa vyombo vya habari akisema sekta hizo ni uchumi wa buluu na pia fedha hizo zitasaidia maendeleo ya uchumi wa buluu unaoendana na mabadiliko ya tabianchi mikoa ya Kanda ya Pwani ya Tanzania, Zanzibar na Bahari ya Hindi.

"Fedha hizi zitasaidia katika mageuzi ya utawala, kujenga uwezo na kuongeza uratibu kati ya wizara. Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira zitaongoza juhudi hizi.

"Pia fedha zitasaidia katika uboreshaji miji, kwa lengo la kukuza maendeleo endelevu hususan katika miji ya Mwanza, Tanga na Pemba. Msaada huu unalenga kuboresha hali ya maisha kwa kuimarisha uendelevu wa mazingira, kuunda fursa za kiuchumi na kuboresha huduma za umma, hasa wanawake na vijana," alisema.

Balozi Grau aliongeza kwamba fedha hizo pia zitagusa jinsia kwa kujikita kuendeleza usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana kwa kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia, kukuza uwezeshaji wa kiuchumi na kusaidia ushiriki wao kiuongozi na michakato ya kufanya maamuzi.

"Pia fedha hizi zitakuza Tanzania kidijitali. Programu hii inalenga kutumia ukuaji wa kidijitali, kwa ajili ya ukuaji wa kiuchumi na kuboresha huduma za umma. Inajumuisha kupanua mtandao wa mawasiliano wa serikali ya Tanzania na kuimarisha hatua za usalama wa mtandao, sambamba na Sheria ya Ulinzi wa Takwimu Binafsi.

"Ukuaji na Upatikanaji wa Fedha, pia ni lengo la fedha hizi ili kuboresha utawala wa fedha na upatikanaji wa fedha. Itaimarisha uhamasishaji wa rasilimali za ndani, kusaidia miundombinu ya soko la fedha na kukuza mazungumzo kati ya sekta ya umma na binafsi, hasa kunufaisha biashara ndogo, za kati, hasa kwa ajili ya wanawake na vijana," alisema.

Alisema msaada wa EU unasisitiza dhamira ya pamoja kwa dira ya maendeleo ya Tanzania na malengo mapana ya kimkakati ya EU.

# Ufinyu wa ardhi kikwazo huduma kwa wagonjwa hospitali ya mkoa

**Na Agustino Kihombo, IRINGA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Afya na UKIMWI imeiagiza serikali kupitia Wizara ya Afya kuharakisha utoaji wa majibu ya agizo lake kuhusu upanuzi wa eneo la Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wagonjwa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Christina Mnzava, alisema hayo jana baada ya kupokea taarifa ya hospitali hiyo kutoka kwa Mganga Mfawidhi, Dk. Alfredy Mwakalebela.

Dk. Mwakalebela alisema kwa sasa hospitali hiyo inakabiliwa na ufinyu wa eneo jambo linalowafanya washindwe kuongeza majengo kwa ajili ya huduma zingine kama upasuaji.

Alisema tayari mchakato wa kuongeza eneo upo katika mamlaka zinazohusika ambapo waliomba kuongezewa eneo kutoka upande wa magereza ihamishwe, jambo ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi.

Aliomba kamati hiyo kulitazama suala hilo kwa jicho la tatu ili waweze kupanua huduma.

"Hospitali yetu imekuwa ikitoa huduma mbalimbali za kibingwa na idadi ya wagonjwa imeendelea kuongezeka siku hadi siku hata kutoka maeneo ya nje ya mkoa wa Iringa, lakini changamoto kubwa hapa ni ufinyu wa eneo, jambo hili tulishalifikisha wizarani, bado linafanyiwa kazi. Hili ni ombi letu kwamba, tuongezewe eneo ili tupanue zaidi huduma," alisema Dk. Mwakalebela.

Alisema ziko baadhi ya huduma ambazo zinahitaji nafasi kubwa, lakini kwa sasa wanalazimika kubanana katika chumba kimoja, jambo ambalo linapunguza ufanisi wa kazi.

Alisema kuwa iwapo serikali itaridhia ombi lao la kuihamisha magereza kama walivyomba, itasaidia kuongeza ufanisi wa kuhudumia wagonjwa.

Akizungumza kwa niaba ya wajumbe wa kamati hiyo iliyofanya ziara mkoani Iringa na kutembelea hospitali hiyo, Dk. Mnzava, alishauri kuanza kufikiria kujenga majengo ya ghorofa ili kulinda rasilimali ardhi waliyo nayo.

"Wakati serikali ikiendelea kushughulikia suala hili la ufinyu wa eneo la hospitali na kutafuta bajeti kwa ajili ya kuhamisha magereza, ushauri wangu ni kwamba kama kuna majengo mapya mnatarajia kujenga fikirieni kuanza ujenzi wa kwenda juu kwa maana ya maghorofa nafasi hii itatusaidia,"alisema Dk. Mnzava.

Changamoto hiyo iliwafanya wajumbe wa kamati hiyo wakiwamo Mohammed Monni na Kassim Hassan Haji kuinyooshea kidole serikal, huku wakitaka kutolewa kwa majibu kwa kuwa ni agizo la kamati lililotolewa tangu mwaka 2023 ilipotembelea katika hospitali hiyo.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Molel, licha ya kukubali uwapo wa changamoto hiyo, alisema katika hospitali hiyo hakuna changamoto ya huduma kwa wagonjwa kutokana na hadhi iliyonayo ya ngazi ya mkoa.

Alisema kila huduma inayohitajika katika hospitali ya rufani ipo tofauti na inavyotafsiriwa sasa.

"Huduma zinazotolewa hapa ni za rufani ngazi ya mkoa kwa hiyo mpaka sasa hakuna changamoto katika utoaji wa huduma kwa nafasi iliyoko, hivyo kinachoelezwa hapa kuhusu ufinyu wa eneo ni suala ambalo linaendelea kufanyiwa kazi, mazungumzo yanaendelea na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi," alisema Dk. Mollel.

Dk. Mollel aliieleza kamati kuwa wizara imeanza kuandaa mchoro kwa ajili ya maboresho ya majengo ya hospitali hiyo ili kujenga majengo ya ghorofa badala ya kuendelea kujenga majengo ya chini hali itakayopunguza mahitaji ya vyumba vya kutolea huduma.

"Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Mbunge, ninaomba mridhie tuendelee na mchakato wa kuanza mpango kabambe kwa ajili ya kuiboresha hospitali hii.

"Mpaka sasa ninapozungumza Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ameshawaagiza wataalam wetu waanze kazi hiyo ambayo tutaiwasilisha kwenu pindi itakapokamilika,"aliahidi.

Licha ya serikali kuwekeza zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya maboresho ya vifaa tiba katika hospitali hiyo, bado inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa wataalamu wa huduma za kibingwa, jambo linalolazimu wagonjwa kuendelea kufuata huduma nje ya Mkoa wa Iringa.

# Watuhumiwa ubakaji binti mbaroni, makundi zaidi yajitokeza na kulaani

**Na Romana Mallya**



WAKATI watu wanaodaiwa kumfanyia ukatili kwa kumlawiti na kumbaka binti, mkazi wa Yombo Dovya, Temeke mkoani Dar es Salaam, wakishikiliwa na vyombo vya dola, makundi zaidi yamezidi kulaani kitendo hicho.

Agosti 4, mwaka huu, katika mitandao ya kijamii, kulisambaa video ikionesha vijana watano wakimfanyia ukatili binti huyo huku wakimrekodi.

Katika video hiyo, vijana hao walisikika wakimtuhumu kutembea na mume wa mtu na binti huyo akisikika kumwomba msamaha mtu aliyetambulishwa kama afande.

Jana, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, alikiambia chombo kimoja cha habari nchini kuwa watuhumiwa hao wanashikiliwa, huku Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stargomena Tax, akisema serikali haitavumilia uvunjwaji wa aina yoyote wa sheria na yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi Nchini, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, uchunguzi wa tukio hilo unaendelea vizuri. Pia aliwataka wananchi kuwa na subira kwa kuwa taarifa itatolewa baada ya kukamilisha yale ambayo sheria zinaelekeza.

"Jeshi la Polisi limekuwa kilipokea simu nyingi kutoka kwa waandishi wa habari wakiuliza tumefikia hatua gani katika uchunguzi wa video iliyosambaa katika mtandao wa kijamii ikionesha tukio la binti aliyefanyiwa vitendo vya ukatili.

"Jeshi la Polisi linatoa wito sote kwa pamoja tuendelee kutafakari namna tunavyoendelea kujadili jambo hili na tunavyotoa maoni katika mitandao ya kijamii na kwenye vyombo vya habari, je, hatuendelei kumtonesha huyu binti majeraha aliyonayo moyoni?

"Je, kwa kuendeleza hayo familia yake hatuendelei kuijeruhi kisaikolojia? Tunaendelea kusisitiza mwenye taarifa za ziada atuwasilishie kwa njia iliyosahihi kwa kutumia mifumo iliyoko bila kuendelea kumuumiza," alisema.

Misime alisema wanawashukuru waliowapa taarifa mbalimbali, akisema huo ndio uzalendo wa dhati wa kuchukia vitendo viovu kama hivyo.

**MADELEKA AWAKA**

Wakili Peter Madeleka, kupitia ukurasa wake wa X, alichapisha barua ya tarehe ya jana iliyo na nembo ya Kampuni yake ya uwakili Stalwart Law Chambers kwenda kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, yenye kumb. Na. SLC/PHQ/IGP/01//2024 yenye kichwa cha habari 'Hitaji la kisheria la kukamatwa kwa watuhumiwa wa ubakaji na ulawiti kwa mwanamke wa Yombo Dovya'.

Barua hiyo ilieleza kuhusu tukio hilo na kurejelea taarifa ya DCP Misime ya kulaani na kwamba linalishughulikia.

"Mpaka leo (jana) hakuna taarifa zozote kuhusu kukamatwa kwa watuhumiwa wa tukio lile licha ya kwamba sura na utambulisho mwingine wa watuhumiwa unajulikana na upo mitandaoni.

"Kwa kuwa chini ya Ibara ya 13 (1) ya Katiba, watu wote ni sawa mbele ya sheria, na kwa kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 26 (1) ya Katiba, kila mtu anao wajibu wa kutii na kuheshimu katiba na sheria za nchi.

"Na kwa kuwa wajibu wa kukamata watuhumiwa siyo hiyari ya polisi, bali ni hitaji la kisheria ambao utaratibu wake umeelezwa katika Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 15 ya Sheria za Tanzania," ilisema sehemu ya barua hiyo.

**UWT, UVCCM WALAANI**

Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) kupitia Mwenyekiti wake, Mary Chatanda umelaani tukio hilo ukisema vitendo vya ulawiti, ubakaji na udhalilishaji kama huo ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na vinaleta athari zinazodumu kwa muda mrefu kwa waathirika.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura namba 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2020 kifungu cha 131(A), tukio hili ni kosa la jinai linalotambulika kama ubakaji wa kundi na adhabu ni kifungo cha maisha.

"Halikadhalika, kifungu cha 154 (C) kumwingilia mtu kinyume cha maumbile ni kosa ambalo adhabu yake ni kifungo cha miaka isiyopungua thelathini," ilisema taarifa ya UWT.

Pia ilisema Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya Mwaka 2015 inakataza kabisa usambazaji wa picha chafu mtandaoni, hivyo kitendo kilichofanywa ni kinyume na sheria na hakipaswi kuvumilika hata kidogo.

UWT ilisisitiza kuwa uchunguzi wa kina na uwajibikaji wa haraka kutoka katika mamlaka zinazohusika ili kuhakikisha haki inatendeka na watuhumiwa wanafikishwa katika vyombo vya sheria. Ilisema msaada wa kisaikolojia unapaswa kutolewa haraka kwa mwathirika wa tukio hilo.

"Watanzania tuna wajibu wa kulinda taswira ya nchi yetu kwa kukemea vikali matukio ya udhalilishaji na ukatili wa aina ile pamoja na kutunza mila na desturi zetu," ilisema taarifa hiyo.

Nao Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) chini ya Mwenyekiti wake, Mohammed Ali Mohammed (Kawaida), umelaani na kukemea vikali tukio la picha mjongeo zinazosambaa mitandaoni zikionesha vijana wakimfanyia ukatili na udhalilishaji mwanamke mmoja."Umoja wa Vijana wa CCM tunawasihi Jeshi la Polisi kuchukua hatua zaidi kuhakikisha wahusika wa tukio hilo wanapatikana kwa haraka na kuchukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria kuhakikisha tukio kama hili halitokei tena kwa jamii ya Watanzania," ilisema taarifa ya UVCCM.

Pia ilitoa kwa jamii kuungana kupinga udhalilishaji na vitendo hivi kwa kuacha kusambaza video na maudhui yanayohusu tukio hilo baya.

**WATAKA WAZIRI AJIUZULU**

Waziri Kivuli wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum wa ACT-Wazalendo, Janeth Rithe, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, alisema chama hicho kinalaani kitendo hicho na kutaka Waziri Masauni ajiuzulu mara moja kwa kile walichokiita kushindwa kazi.

"Tunalitaka Jeshi la Polisi lifanye uchunguzi haraka kuhusu tukio hilo na wahusika wote wachukuliwe hatua za kisheria," alisema.

Jana, katika ukurasa wake wa X, Boniface Jacob, alichapisha maelezo yanayodai kwamba, watuhumiwa hao wamekamatwa wapo chini ya ulinzi.

# Wadau waomba kuondolewa VAT vifaa vya nishati safi

**Na Mwandishi wetu**

WADAU wa nishati safi ya kupikia wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kwenye vifaa vya kutengenezea nishati hiyo ili watu wengi wamudu gharama.

Wakizungumza jana wakati wa mjadala wa nishati safi ulioandaliwa na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) kupitia Mpango wa CookFund na kufadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), walisema iwapo kodi itaondolewa, Watanzania wengi watamudu gharama ya nishati hiyo.

Walisema Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa nishati safi ya kupikia, amelenga kuwa ifikapo 2034 asilimia 80 ya Watanzania wafikiwe na nishati safi na tayari kuna mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia 2024-34.

Akijibu ombi hilo, Kamishina Msaidizi wa Sera, Wizara ya Fedha, Dk. Remidius Ruhinduka, alisema serikali inathamini maoni ya wadau wa sekta ya nishati safi wanayoyatoa katika kuhakikisha kuwa ajenda ya mpango wa taifa wa nishati safi unafanikiwa.

Alisema serikali imedhamiria kuona mpango huo, malengo yake yanafikiwa na maoni ya wadau ni sehemu ya utekelezaji wa ajenda hiyo.

Dk. Ruhinduka alisema mijadala ya wadau inasaidia katika kukumbushana katika kuchukua hatua na kuharakisha azma ya serikali ya kuona asilimia kubwa ya Watanzania wanaachana na matumizi ya nishati chafu ili kulinda mazingira na afya zao.

Alisema serikali kupitia sera mbalimbali ikiwamo sera ya mazingira na misitu inahamasisha mpango huo, na ndio maana Rais Samia alizindua mkakati wa taifa wa kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ifikapo 2034.

Kwa mujibu wa Dk. Ruhinduka, serikali imeweka mipango mbalimbali ya kimkakati ukiwamo kuhakikisha gharama za ununuzi wa teknolojia ya nishati safi zinapungua ifikapo mwaka 2026.

"Lakini juhudi nyingine zilizochukuliwa na serikali ni pamoja na kuondoa VAT kwenye mitungi yote ya gesi ya asilia (LPG) inayoingia nchini ili kuhakikisha bei inakuwa nafuu kwa watumiaji.

"Lakini jitihada nyingine ni pamoja na upatikanaji wa huduma za umeme vijijini, na ifikapo mwakani vijiji vyote vitakuwa na umeme," alisema.

Ofisa wa Umoja wa Ulaya (EU) anayehusika na nishati, Max Peddretti, alisema wamefadhili mjadala huo kwa wadau ili kubadilishana mawazo kati ya serikali na sekta binafsi na kuona namna utekelezaji wa mpango huo wa taifa utakavyokuwa na mafanikio na kupunguza gharama za upatikanaji wa nishati safi.

Alisema ununuzi wa teknolojia ya nishati safi ni gharama, lakini matumizi yake ni rahisi sana ukilinganisha na matumizi ya mkaa katika mapishi ya kila siku.

Aidha, alisema EU inapenda kuona Watanzania wanamudu kununua teknolojia ya nishati safi, ikiwamo majiko ya kupikia ili kulinda afya ya watumiaji na kuweka mazingira safi.

Naye Mkuu wa Idara ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira katika Ubalozi wa Uingereza, Catherine Pye, alisema mjadala huo ungependa kuona vifaa muhimu kama vile majiko ya umeme (induction) vinapatikana kwa gharama nafuu ikiwa jitihada zitachukuliwa ikiwamo pendekezo kwa serikali kuangalia namna ya kupunguza gharama ya kodi na VAT katika vifaa hivyo.

Alisema Uingereza imefanikiwa kwa sababu imekuwa na utaratibu wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ikiwamo serikali kutoa umeme wa jua kwa wananchi, na wanaunga mkono juhudi za Rais Samia katika kuwezesha matumizi ya nishati safi kwa kutoa misaada mbalimbali ikiwamo majiko ya kupikia katika shule 200 hapa nchini.

Ofisa Uwekezaji Mwandamizi wa UNCDF, ambao waliandaa mjadala huo kupitia ufadhili wa EU, Abraham Byamuru, alisema lengo ni kusapoti jitihada za serikali katika mpango mkakati wa miaka 10 wa kutumia nishati safi nyumbani na kwenye taasisi.

Alisema wadau mbalimbali wakiwamo wa wizara ya fedha, wataalamu wa kodi kutoka Mamlaka ya Kodi (TRA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wauzaji wa vifaa hivyo wamekutana ili kujadili utekelezaji wa mkakati huo kwa mafanikio zaidi.

"Kodi ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, lakini matumizi ya nishati safi kwa kiasi kikubwa yatasaidia kulinda misitu na afya za watu pia. Tumefurahi kuona serikali ipo tayari kupokea mapendekezo yetu, lakini imetutaka kuja na tathmini kuona ni faida gani zitapatikana endapo kodi zitapungua," alisema.

**Kwa mujibu wa Dk. Ruhinduka, serikali imeweka mipango mbalimbali ya kimkakati ukiwamo kuhakikisha gharama za ununuzi wa teknolojia ya nishati safi zinapungua ifikapo mwaka 2026.**


Air Tanzania
Training Centre




**KOZI YAWAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW)**

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Centre ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 01 Octoba 2024. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam(JNIA) Terminal One kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwahapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 26 Agosti 2024.

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Muomaji asiwe na michoro yoyote ya kudumu inayoonekana mwilini (tattoos)
iii. Awe mwenye akili timamu, mwenye urefu kuanzia futi 5"4 (162 cms) na kuendelea.
iv. Elimu ya kidato cha nne, mwenye ufaulu angalao masomo manne kwa alama "D", likiwemo somo la Kiingereza na Jiografia
v. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
vi. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa na kusoma nchini. **Angalizo: Waombaji kutoka nchi za kigeni watatakiwa kulinganisha matokeo ya vyeti vyao kwenye Baraza la Mitihani Tanzania (NACTE) yafanane na matokeo ya Tanzania.**

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na vyeti vingine vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV

**Maombi yatumwe kwa:**
**Mkuu wa Chuo,**
**ATCL Training Center**
**Box no 543**
**Dar Es Salaam**
**Email, training@airtanzania.co.tz**

**Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali piga namba hizi TU:**
**Mob: +255754 345 874, +255735 787212**

*ATCL TRAINING CENTER*
*"FULFILL YOUR FLYING DREAMS WITH US"*

HABARI KITAIFA

## Hakimu ataka mawakili kutumia lugha ya staha

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kujeruhi inayowakabili wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54), umekataa kuahirishwa kesi kwa madai kuwa wakili wa utetezi anataka kuchelewesha kwa kudai kuwa anashida ya kiafya.

Aidha, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam iliomba pande zote mbili katika kesi hiyo kutumia lugha za kuheshimiana ndani ya chumba cha mahakama kwa sababu kuna watu wanajifunza kutoka kwao.

Ombi hilo liliwasilishwa jana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Aaron Lyamuya, wakati shahidi Kiran Ratilal akiulizwa maswali ya dodoso na Wakili wa Utetezi, Edward Chuwa.

Mwanga alifikia hatua hiyo baada ya Wakili Chuwa kuomba ahirisho la maswali ya dodoso kwa shahidi Ratilal kwa madai kuwa hawezi kuendelea kwa sababu ya afya yake na pia kuna dawa za kutumia.

Mwanga alidai kuwa hawawezi kukubali ahirisho kwa sababu wakili huyo alitakiwa kulisema hilo mapema kabla kesi haijaanza kusikilizwa kuwa ikifika muda fulani waahirishe.

"Jamhuri hatuwezi kukubali, wakili alitakiwa kulisema hili mapema anachokifanya ni kutaka kuchelewesha kesi hatuwezi kukubali amalize maswali ya dodoso kwa shahidi."

"Mara ya mwisho alisema anaenda Mahakama Kuu, lakini alivyotoka nje alikuwa anazungumza na media na pia hakusema anaenda kwenye kesi gani," alidai Wakili Mwanga.

Hata hivyo, Chuwa alidai kuwa siku hiyo hakusema anakwenda Mahakama Kuu, alidai kuna kazi anakwenda kuifanya na pia alihoji alikuwa akizungumza na media saa ngapi?

"Naenda kuonana na daktari katika Hospitali ya Hindul Mandal na siku ya kesi ninaweza kuja na ushahidi hapa mimi nina umri wa miaka 60, nimeomba ahirisho kwa sababu ya ugonjwa," alidai Wakili Chuwa.

Hakimu Lyamuya alisema suala la ugonjwa halipo kwenye nafasi ya kukataa au kukubali ni mtu mwenyewe anavyojisikia.

"Kwa sababu umesisitiza kwa umri wako wa miaka 60, mahakama inaahirisha kesi hii kwa nafasi ya mwisho ya kufanya maswali ya dodoso ni haki yako, lakini inatakiwa ifike mwisho," alisema Hakimu Lyamuya.

Pia, Hakimu Lyamuya aliwataka watumie lugha ya kuheshimiana wanapouliza maswali kwa sababu ni watu wengi wanasikiliza, lakini pia kuna wanafunzi wa sheria ambao wanajifunza kila kitu kutoka kwao.

Hakimu Lyamuya alifikia hatua hiyo, baada ya Wakili Chuwa kumtuhumu Wakili Mwanga kuwa anamsaidia shahidi, hii ni baada ya kupinga kitendo cha shahidi wake kuulizwa swali ambalo tayari alishalijibu.

"Mheshimiwa hayo ni maneno gani? Mimi sijamsaidia shahidi nimepinga shahidi kuulizwa swali hilohilo ambalo tayari alishalijibu," alidai Mwanga.

Kesi imeahirishwa hadi Agosti 15, 2024 kwa ajili ya upande wa utetezi kuendelea kumuuliza maswali ya dodoso shahidi.

Nathwan pamoja na mke wake Sangita Bharat (54) wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana Dar es Salaam, wanatuhumiwa kwa mashtaka manne likiwamo la kujeruhi waliyoyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.

# TAKUKURU yaridhishwa na ujenzi barabara

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

KAMANDA wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Ruvuma, Hamza Mwenda, amepongeza Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) mkoani humo kwa kufanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya barabara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Mwenda alitoa pongezi hizo jana wakati wa utiaji saini mikataba ya matengenezo ya barabara za vijijini na mjini kati ya TARURA na makandarasi mkoani Ruvuma kwa mwaka wa fedha 2024/2025 iliyofanyika kwenye viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.

Mkuu wa Mkoa huo, Kanali Ahamed Abbas Ahmed, alisema kuwa mikataba iliyosainiwa jana itakwenda kufanya kazi kwa viwango vinavyokubalika kwa kila mpenda maendeleo wa Mkoa wa Ruvuma na katika kipindi cha mwaka jana TARURA walifanya kazi nzuri licha ya kuwapo kasoro ndogo ambazo zilishafanyiwa kazi.

Alisema makandarasi walioingia mikataba ya kutengeneza miundombinu ya barabara katika kipindi cha mwaka 2024/2025 wanapaswa kufanya kazi kwa weledi.

Mwenda aliitaka TARURA kusimamia kikamilifu miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, kabla ya kuwalipa fedha makandarasi wanapaswa kwenda maeneo ya miradi ili malipo yafanyike kuepuka malipo hewa. Meneja wa TARURA mkoani Ruvuma, Mhandisi Silvester Chinengo, alisema mwaka wa fedha 2024/2025 wameidhinishiwa Sh. bilioni 22 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja kwenye mtandao wao na katika kiasi hicho cha fedha Sh. bilioni 7.89 zinatoka kwenye mfuko wa barabara, Sh. bilioni 4.5 zinatoka Mfuko Mkuu wa serikali kwa maana ya mfuko wa majimbo na Sh. bilioni 9.79 zinatoka kwenye tozo ya mafuta.

Alisema bajeti hiyo itaenda kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 1,145.73, kujenga madaraja 50 na makaravati 57 na mpaka sasa TARURA imekamilisha mikataba ya ununuzi 50 ambayo ni ya awamu ya kwanza yenye gharama ya Sh. bilioni 14.7.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma alisema ni hatua kubwa kwa maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma kuwa na matarajio makubwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara, madaraja na makaravati kwa kuwa uchumi wa nchi unategemea miundombinu ya barabara.

Baadhi ya makandarasi walio hudhuria hafla hiyo wameishukuru serikali kwa jitihada zinazofanywa za kuhakikisha kuwa miundombinu ya barabara inatengenezwa kutoka mjini mpaka vijijini ili kusaidia wakulimakusafirishamazaoyao kutoka shambani hadi majumbani mwao kwa urahisi zaidi.



Bharat Nathwani (kulia) na mke wake, Sangita Nathwani (kushoto), wakiingia katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi ya kumjeruhi jirani yao inayowakabili. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kamati yavutiwa viwango huduma bobezi Muhimbili

**Na Christina Mwakangale**

KAMATI ya Ustawi wa Jamii kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imesema imevutiwa na viwango vya utoaji huduma bobezi na za kibingwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), husani huduma ya VIP.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Sabiha Filfil Thani, ambaye ni Mwakilishi wa Viti Maalumu Kundi la Wazazi, Mkoa wa Kusini Unguja, alisema hayo jana baada ya kamati na wajumbe wake kutembelea hospitali hiyo jijini Dar es Salaam.

Alisema lengo la kufanya ziara hiyo ni kujifunza namna ya utoaji huduma za bima ya afya, baada ya Wizara ya Afya Zanzibar kupitisha Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya na kwamba huduma ya watu mashuhuri (VIP) kwa wagonjwa inayotolewa na MNH, ni ya kuigwa.

"Tumekuja kuona namna wenzetu walipofikia kupitia Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na jinsi wanavyofanya kazi zao, ili kamati tuweze kuishauri serikali. Tutakaporudi tunaenda kuishauri serikali ili kuwapo huduma bora.

"Zanzibar tuna hospitali 10 za wilaya ambazo zinafanya kazi vizuri na moja ni ya mkoa. Tunataka kuona namna MNH mlivyopiga hatua na sisi tujiweke sawa, ili afya za Watanzania ziwe bora zaidi. Tunatamani huduma hii ya VIP tuanze kuitoa hivi sasa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, alisema ujumbe huo kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni muhimu ikizingatiwa upo mkataba kati yake na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kushirikiana kuhudumia wagonjwa wanaofika hospitalini hapo ambao wangepelekwa nje ya nchi.

"Tuna matibabu mengi bobezi, kupandikiza uloto, vifaa vya usikivu na tiba ya figo, ushirikiano huu na wenzetu umesaidia kupunguza gharama kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzaniakwaujumla.Bimaya Afya kwa Tanzania bara ina kama miaka 12.

"Kuna uzoefu, mafanikio, changamoto hivyo ni sehemu sahihi wao kuja kujifunza na kwa nini Muhimbili kwa sababu, tunapokea wagonjwa wengi zaidi kuliko hospitali yoyote Tanzania kwa wagonjwa wa bima ya afya kila siku tunaona wagonjwa 4,000 na tunao 2,000 ambao wamelazwa," alisema Prof. Janabi.

Mkuu wa Idara ya Tiba na Magonjwa ya Dharura MNH, Dk. Juma Mfinanga, aliwaambia wajumbe wa kamati hiyo kwamba, kuanzishwa huduma za dharura kwa watoto kwenye idara hiyo, kumepunguza vifo kwa asilimia 45.

"Ukiboresha tiba ya dharura kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), unaweza kupunguza vifo kwa zaidi ya asilimia 45 na ndicho hospitali hii inakifanya katika kuboresha, kuokoa maisha ya watoto wengi," alisema.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaotumia mitandao vibaya wadhibitiwe

**MAPAMBANO** dhidi ya uhalifu mitandaoni ni jambo muhimu hasa wakati dunia ikiwa kwenye mabadiliko ya kutumia teknolojia ya mawasiliano.

Kuna mambo mengi yanayotokea katika kipindi hiki huku wahalifu wakitafuta mbinu mbalimbali za kuhakikisha wanakwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Dunia inapokwenda sambasamba na mabadiliko ya teknolojia kunarahisisha kazi na kupunguza muda unaotumika kwa binadamu kuifanya kazi hiyo.

Hata hivyo, kuna watu wanaotumia fursa hiyo kujinufaisha na kuona hawaachwi nyuma kwa jambo lolote lile.

Miaka ya nyuma kabla ya teknolojia ya mawasiliano haijabadilika, kazi nyingi zilikuwa zikifanyika kwa kwenda sehemu husika, lakini sasa hivi mtu anaweza kukaa nyumbani na akamaliza kila kitu kwa kutumia simu yake ya mkononi.

Siku za nyuma sehemu zenye huduma muhimu kama ulipaji wa bili za umeme, maji na benki, mtu ilibidi aende kwenye ofisi hizo hali iliyokuwa ikisababisha msongamo mkubwa wa watu.

Sasa hivi hata ukiwa nje ya nchi unaweza kufanya miamala na kulipia bili zako kwa wakati.

Kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi ilikuwa inachukua muda kumtumia ndugu yake pesa, lakini kwa sasa teknolojia imerahisisha, hakuna usumbufu tena.

Lakini, teknolojia hiyo imeingiliwa na kutumika vibaya kwa baadhi ya wahalifu kwenye sekta ya fedha kwa kuwaibia watumiaji na kuwafanya waogope kuitumia.

Mamlaka ya Mawasiliano Nchini (TCRA), imeeleza wazi kuwa inaendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti uhalifu unaofanyika mitandaoni, ikiwamo huduma za kifedha kutokana na kuongezeka kwa mifumo mipya ya mawasiliano ya teknolojia.

Inapokuja teknolojia mpya ni muhimu ikatumika vizuri ili kunufaisha watu na kuondoa ugumu uliokuwapo mwanzo.

Kwa nchini Tanzania, wafanyabiashara, wajasiriamali wamerahisishiwa kazi kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano ambapo kwa sasa wanaweza kutuma pesa nje ya nchi na kuletewa bidhaa wanazotaka badala ya kusafiri hali inayowapunguzia gharama.

Katika matumizi ya teknolojia hii pia kunahitajika uaminifu wa hali ya juu ndio maana hata TCRA ikiwa ni mdhibiti wa matumizi mabaya ya mawasiliano imekuwa ikiingilia kati, kila inapoona mambo hayaendi sawa.


Kuna wanaotumia teknolojia hiyo kwa malengo mabaya ya kuwachafua watu wengine kwenye mitandao.

Hali hiyo imekuwa ikishamiri kwenye mitandao ya kijamii kiasi cha kuharibu hali ya hewa na wengine wanaochafuliwa huathirika kisaikolojia.

Viongozi wa juu wanapokuwa kwenye majukwaa wamekuwa wakikemea tabia hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa kama isipodhibitiwa itarudisha nyuma maendeleo.

Hivyo basi, mabadiliko ya teknolojia hayawezi kuepukika duniani hivyo ni muhimu wadhibiti uhalifu mitandaoni wanapaswa kuwa makini kudhibiti hali hiyo ili kuepuka matumizi mabaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Morogoro ongezeni kasi sekondari mkoa wenu

Na Sabato Kasika

**SAYANSI** ni moja ya masomo ambayo kwa muda mrefu yanakimbiwa na baadhi ya wanafunzi wasichana kutokana na dhana iliyojengeka miongoni mwao kuwa ni magumu hasa pale yanapohusisha na hesabu.

Ili kuondoa dhana hiyo, kuna jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali pamoja na wadau wa elimu, kuanzia kutoa motisha, kuongeza shule za sayansi na kuhamasisha wasichana kupenda masomo hayo na kuelezwa kuwa siyo magumu kama wanavyodhani.

Jitihada za hivi karibuni ni ujenzi wa shule za sekondari za wasichana za masomo ya sayansi kila mkoa, kupitia mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Hatua hiyo, inalenga kuifanya idadi ya wanafunzi wa kike iwe sawa na wavulana katika masomo hayo ili hatimaye kuwe na wataalamu wengi wa kike wa fani mbalimbali kama walivyo wa kiume.

Hadi kufikia sasa, sekondari 25 zimeshajengwa katika mikoa 25 na zimeanza kupokea wanafunzi, huku mkoa mmoja ambao ni Morogoro, ukiendelea na kazi ya ukamilishaji wa sekondari hiyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa ndiye aliyasema hayo hivi karibuni, akifafanua kuhusu hatua ambazo zimechukuliwa na serikali.

Katika ufafanuzi wake, anasema serikali ilishatoa Sh. bilioni 104 kati ya Sh. bilioni 106.6, zilizotengwa kwenye bajeti, kwa ajili ya ujenzi wa shule sekondari hizo ambayo ni sawa na asilimia 98.

Binafsi, ninaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na serikali za kutaka kuhakikisha wasichana wanapata fursa ya kusoma masomo ya sayansi ambayo kwayo muda mrefu wamekuwa wakiyakwepa.

Hatua hiyo inayochukuliwa na serikali, inalenga kuwafanya wasichana wawe na ujuzi katika sayansi, teknolojia na ubunifu, hasa kwenye dunia hii ya sasa ambayo tunashuhudia mabadiliko mbalimbali ya kimaendeleo.

Hongera kwa mikoa 25 ambayo imekamilisha ujenzi wa sekondari hizo za wasichana na kuanza kuchukua wanafunzi, lakini Mkoa wa Morogoro uongeze kasi ili ukamilishe sekondari hiyo.

Matarajio ya serikali na wadau wa elimu, ni kuona nchi inapiga hatua katika masomo ya sayansi, kwa wasichana ili walete ushindani kwa wenzao wa kiume ambao kwa muda mrefu wamekuwa mstari wa mbele.

Jitihada za ujenzi wa shule hizo ni kuleta usawa wa kijinsia kwa wasichana katika kusomea masomo ya sayansi ili baadaye wapewe fursa za ubunifu au maendeleo kama ilivyo kwa wanafunzi wa kiume.

Vilevile, hatua zilizochukuliwa na serikali za kujenga sekondari za wasichana za masomo ya sayansi, zinaonesha kuwa dhana ya kuwa masomo ya sayansi ni magumu kwa wasichana haina nafasi tena.

Hivyo, ukamilishaji wa sekondari hizo ni hatua muhimu kwa malengo ambayo serikali imejiwekea ya kuinua wasichana kupitia masomo ya sayansi, ndio maana nikashauri Mkoa wa Morogoro nao uharakishe kukamilisha sekondari ya mkoa kama ilivyo kwa mikoa mingine 25.

Nguvu kubwa kwa sasa imeelekezwa katika kuwahamasisha wasichana kusoma masomo ya sayansi ili kutengeneza usawa, kwa kuweka hamasa katika masomo hayo, ni vyema hilo lingezingatiwa na kila mkoa.

Mkoa wa Morogoro ongezeni kasi, ama jifunzeni mbinu zilizotumiwa na mikoa mingine ili muweze kukamilisha ujenzi huo kwa muda mwafaka.

Ingependeza kama mkoa utakwenda sawa na kasi ya serikali ya kuboresha elimu, hasa ya ujenzi wa sekondari hizo ili kuongeza ufaulu wa masomo ya sayansi na TEHAMA kwa wasichana.

HABARI KITAIFA

# FCS, TCRA CCC zatia saini makubaliano kulinda watumiaji mawasiliano

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Foundation for Civil Society (FCS) na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA CCC) zimetia saini makubaliano ya miaka mitatu ya kuimarisha juhudi za kulinda haki za watumiaji wa huduma katika sekta ya mawasiliano nchini Tanzania.

Ushirikiano huo unalenga kuwalinda watumiaji dhidi ya mbinu za kibiashara zisizo za haki katika soko, kuhakikisha kunakuwapo haki na uwajibikaji katika kutoa huduma kwa watumiaji na kuwawezesha kufanya uamuzi sahihi wanaponunua na kutumia bidhaa au huduma hizo.

Akizungumza wakati wa utiaji saini wa makubaliano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa FCS, Justice Rutenge, alisema upo umuhimu kwa asasi za kiraia kushiriki katika kuimarisha mifumo ya kulinda na kutetea haki za watumiaji wa huduma na bidhaa.

"Kwa miaka mingi FCS imekuwa ikisisitiza maendeleo yaliyojikita kuwanufaisha wananchi na kuwaweka mstari wa mbele. Nafasi na utayari wetu katika ulinzi wa watumiaji wa huduma na bidhaa vinavyotokana na dhana hiyo na tuna lengo la kukuza mifumo thabiti ya kulinda watumiaji wa huduma na bidhaa kwa kuzishirikisha asasi za kiraia," alisema Rutenge.

"Tunategemea sauti kutoka asasi za kiraia nchini katika kuwatetea watumiaji na kuleta mabadiliko chanya katika kulinda haki zao kwa sababu tunaamini kwamba zina nafasi kubwa katika ushawishi kwenye masuala muhimu ya kitaifa."

Rutenge alisema watumiaji wana haki ya kupata suluhu ya haki kwa madai ya msingi, elimu na uwezo kuhusu bidhaa, huduma, uhakika wa ubora wa bidhaa na huduma.

"Kwa hiyo tutashirikiana na TCRA CCC, kwa kuwa lina dhamana la kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano ili kukuza uwezo wao katika kuimarisha ulinzi na haki za watumiaji," alisema Rutenge.

Alisema kulinda haki za watumiaji kunachangia maendeleo ya masoko na ukuaji wa biashara na zinazoheshimu sera za kulinda watumiaji na kuwapa wateja wao kipaumbele hujijengea hadhi na kuziweka katika nafasi nzuri kiushindani.

"Katika soko la sasa lenye mabadiliko ya haraka, uadilifu katika biashara unategemea kwa kiasi kikubwa kulinda haki za watumiaji dhidi ya mbinu zisizo za haki na udanganyifu katika biashara. Wafanyabiashara wana nafasi muhimu katika kuhakikisha uwazi na usahihi katika shughuli zao, kutoa taarifa sahihi na kwa wakati na kuepuka upotoshaji kuhusu bidhaa na huduma zao," alisema Rutenge.

Katibu Mtendaji wa TCRA CCC, Mary Msuya, alisema katika mazingira ya ukuaji wa sekta ya mawasiliano, suala la kuwalinda watumiaji lina umuhimu mkubwa kuwajengea uwezo watumiaji ili wawe na uelewa wa haki zao, wajibu na fursa mbalimbali zilizopo katika seka hiyo ili washiriki katika yale ya msingi yanayowahusu.

"Ushirikiano kati ya TCRA CCC na FCS utatoa mchango kwa watumiaji wa makundi mbalimbali ikiwamo wanawake, vijana, wajasiriamali na wenye mahitaji maalumu kwa kuwaelimisha na kuwajengea uwezo wa utambuzi wa masuala muhimu yanayowahusu ili wawe na mchango wanapotumia huduma na bidhaa za mawasiliano," alisema Mary.

Alisema baraza linaamnini kuwa watumiaji wenye uelewa wanafanya uamuzi sahihi wanapotumia huduma na bidhaa za mawasiliano na kuwa na uwezo wa kuwawajibisha watoa huduma ili kupata bora, zenye viwango na zinazokidhi mahitaji yao.




Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdurahman (wa tatu kushoto) na viongozi wenzake wakiwa kwenye kaburi la Waziri Mkuu mstaafu, Hayati Edward Lowassa, baada ya kuweka shada la maua, walipolitembelea wakati akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Monduli, mkoani Arusha juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwanasaikolojia: Wanaopiga 'chabo' wana tatizo la akili

**Na Christina Mwakangale**

MWANASAIKOLOJIA tiba kutoka Somedics Polyclinic Health Centre Dar es Salaam, Saldin Kimangale, ameeleza tatizo linalowapata baadhi ya watu la kupiga 'chabo' akiwataja kukumbwa na ugonjwa wa akili 'Voyeurism'.

Ugonjwa wa kupiga chabo kwa kutaka kushuhudia mtu aliye faragha (Voyeurism), ndio unaowakumba watu hao akisema ni tatizo la akili, ambalo humpa msukumo mtu kuwa na mawazo ya ngono yenye nguvu na kujirudia rudia mara kwa mara.

Kimangale aliyasema hayo, akizungumza na gazeti hili na kufafanua dhana hiyo iliyomo kwa baadhi ya wanajamii, akisema watu hao muda wote huwa na hamu au tabia zinazohusisha kuchungulia watu bila wao wenyewe kujua ambao wako utupu, wakiwa wanabadili nguo, kuoga au wanaofanya tendo la ndoa.

Kimangale alisema kwamba ili kuelimisha umma na kutokana na tukio lililotokea mkoani Tabora, baadhi ya wanawake waliokuwa wanapata huduma ya kujifungua kwenye Zahanati ya Isevya, iliyopo Manispaa ya Tabora, kudai kwamba wanachunguliwa wanapojifungua.

Wiki hii, vyombo vya habari vimeripoti kwamba, wanawake hao wameiomba serikali kujenga uzio mrefu kuzunguka zahanati hiyo, ili kukomesha watu wasio na maadili wanaowachungulia hasa wenye rika la ujana.

Alisema pamoja na sababu za uwazi uliopo katika mitandao ya kijamii, kumekuwapo na wimbi kubwa la hali zinazoweza kutambuliwa kama 'parafilia' ikiwamo kujionesha sehemu za siri, kuangalia picha au picha mjongeo za watu walio utupu.

"Hata hivyo, utambuzi wa hali hii, unasisitiza zaidi kuhusisha watu halisi na wala sio picha au video. Ifahamike pia, mitandao ya kijamii takribani yote inawezesha kumuona mtu mubashara.

"Hii ndio kusema kuwa pengine kuna idadi kubwa ya watu wenye magonjwa ya parafilia ikiwamo huu ugonjwa wa 'Kupiga Chabo'. Kwenye jamii nyingi, tatizo hili limeenea zaidi kwa wanaume kuliko wanawake," alifafanua.

**VIGEZO VYA UTAMBUZI**

Kimangale alisema kwa mujibu wa Kitabu cha Mwongozo wa Uchunguzi na Takwimu za Matatizo ya Kiakili (DSM-5), ugonjwa wa kupiga chabo unatambuliwa pale ambapo mwathirika anapokuwa na hali zifuatazo:

"Mawazo ya mara kwa mara na yenye nguvu ya kujisikia kimapenzi kutokana na kuchungulia mtu aliye faraghani ambaye yuko uchi, anapovua nguo, au anaposhiriki ngono.

"Iwapo hali hii inaingilia utendaji kazi wake, kwa sababu ya mawazo/ fikra, dhiki na athari anazozipata kwa kujishughulisha na tabia hii.

**VYANZO NA SABABU**

Alisema zipo sababu kadhaa na changamoto za tatizo hilo hazijulikani bado, lakini zinaweza kuhusisha mchanganyiko wa mambo ya kisaikolojia, kijamii na kibaiolojia.

"Uzoefu wa utotoni, mafundisho ya kijamii na tabia fulani za kibinafsi zinaweza kuchangia katika kukua kwake. Unyanyasaji wa kijinsia, matumizi mabaya ya dawa na kujishughulisha na ngono kupita kiasi zinatajwa kuwa baadhi ya vichocheo vya tatizo hili.

**MATIBABU**

Kuhusu matibabu mwanasaikolojia huyo alisema, ugonjwa wa kuchungulia mara nyingi hujumuisha matibabu ya akili.

"Tiba za kisaikolojia kama vile tiba ya kitabia na utambuzi (CBT), inayolenga kuelewa na kudhibiti hamu, misukumo, mawazo ya kufikirika na tabia za msingi.

"Mtoa huduma atazingatia kuimarisha uwezo wa kuhusiana na jamii na uwezo wa kusikiliza. Kwa baadhi ya waathirika, dawa zinazopunguza msisimko wa ngono au kutibu hali nyingine zinazoambatana zinaweza kupendekezwa.

**SHERIA NA MAADILI**

Alisema kuchungulia watu wakiwa utupu bila ridhaa yao ni kinyume cha sheria.

"Ni kuingilia faragha za watu kitu ambacho kinaweza kupelekea kuchukuliwa hatua katika maeneo mengi wakati unahusisha uvamizi wa faragha, au uchunguzi usio na ridhaa.

"Matokeo ya kisheria yanaweza kujumuisha mashtaka ya jinai na adhabu. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema:

Ibara ya 16 ya Katiba ya Tanzania inasema wazi kuwa:

"Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafasi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi," alifafanua.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Samia Legal Aid kuhamasisha ongezeko mawakili

**Na Mwandishi Wetu**

MPANGO wa Msaada wa Sheria wa Rais Samia Suluhu, maarufu kama Samia Legal Aid Campaign, umesema utahamasisha wanafunzi wengi wa sheria wanaomaliza vyuo kujiunga na Shule Kuu ya Sheria Tanzania ili kuwa na mawakili wengi kwa ajili ya kutetea haki za watu.

Mkurugenzi wa Ufuatiliaji Haki wa Wizara ya Katiba na Sheria, Beatrice Mpembo, alisema jana mkoani Morogoro katika ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan. Mkurugenzi huyo na wanasheria wengine kutoka wizara hiyo wako katika ziara hiyo.

Alisema kwenye ziara hiyo wamekuwa wakichukua changamoto mbalimbali za wananchi kwa ajili ya kwenda kuzifanyia kazi, nyingi zikiwa migogoro inayohitaji kutatuliwa kwa kufuata sheria.

Mpembo alisema iwapo wanafunzi wengi watahamasika kusoma kwenye shule hiyo ya sheria kwa vitendo, Tanzania itapata wanasheria wengi na kuwezesha upatikanaji wa mawakili kuwa rahisi kwa wananchi wa kawaida.

"Timu yetu ya msaada wa sheria kwenye ziara hii ya mheshimiwa Rais inaainisha maeneo yanayohusu haki mbalimbali za kikatiba kwa lengo la kuishauri serikali ili kila mwananchi aweze kuzipata haki hizo kwa urahisi na kwa usawa," alisema.

Mpembo alisema Rais Samia alipotembelea Chuo Kikuu Mzumbe mkoani humo, timu ya Mama Samia Legal Aid ilipata fursa ya kuainisha maeneo ya ushirikiano kati ya Wizara ya Katiba na Sheria na chuo hicho.

"Eneo mojawapo ni kuhamasisha wanafunzi wanaomaliza chuo hicho na vingine kujiunga na LST ambayo iko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ili kupanua wigo wa kupata wanasheria wa kutosha ambao wizara itawatumia kwenye kampeni hii ya Samia Legal Aid," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mpaka kukamilika kwa ziara hiyo ya Rais, wananchi wengi watakuwa wamenufaika na msaada wa kisheria ambao wamekuwa wakiutoa kila eneo ambalo Rais Samia ametembelea.

"Tumekutana na wananchi wengi sana na wamefurahi kupata elimu ya msaada wa sheria na wengine wametupa changamoto zao ambazo tumezichukua na kwenda kuzifanyia kazi na wananchi kwa ujumla wamefurahia sana ziara hii ya mheshimiwa Rais Samia," alisema Mpembo.

Alisema Mama Samia Legal Aid ni kampeni endelevu yenye lengo la kuwapatia wananchi elimu ya msaada wa sheria na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili kwa wale ambao hawana uwezo wa kuweka mawakili kwenye mashauri yao.

Kaimu Mkrugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Ester Msambazi, alisema wananchi wanapopata elimu ya kisheria na ushauri, wanakuwa na uwezo wa kuelewa taratibu za kisheria na haki zao, hivyo kupunguza malalamiko na migogoro isiyokuwa na ulazima.

"Kampeni hii inalenga kusogeza huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi kwa njia rahisi na ya karibu. Kupitia kliniki za ushauri na elimu ya sheria, wananchi watapata fursa ya kushauriwa na wataalamu wa sheria bila malipo," alisema.

Alisema kampeni hiyo inalenga pia kujenga jamii yenye ufahamu zaidi na yenye uwezo wa kudai na kulinda haki zao za ardhi kwa mujibu wa sheria kukuza usawa na haki katika jamii, kuheshimu matakwa ya marehemu, kuzuia migogoro ya mirathi na kusimamia mali kwa njia inayofuata sheria na haki za kila mmoja.

Mama Samia Legal Aid Campaign ilianza kutekelezwa Aprili mwaka jana kwa kuanzia mkoani Dodoma na mpaka sasa tayari mikoa saba imefikiwa. Mbali na Dodoma, mikoa mingine iliyofikiwa ni Manyara, Singida, Simiyu, Shinyanga, Njombe na Ruvuma.

Tangu ilipozinduliwa Aprili, mwaka jana, jijini Dodoma, imeshawanufaisha zaidi ya wananchi 494,000 kutoka katika mikoa saba, ambao wamepata suluhisho la migogoro huku migogoro ya ardhi ikiwa inaongoza.

Kampeni hiyo imeshafikia mikoa saba, halmashauri 42, kata 452, na vijiji/mitaa 1,348 ambayo imewagusa wananchi kwa kuwapa msaada wa kisheria bure miongoni mwao wakiwamo wafungwa na mahabusu.






## Naibu Waziri ataka viwango mwendokasi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, ameitaka kampuni ya M/S Sinohydro Cooperation Limited inayojenga miundombinu ya mfumo wa usafiri wa mabasi yaendayo haraka kuhakikisha inajengwa kwa viwango vya kimataifa.

Kampuni hiyo inajenga mfumo wa tatu wa barabara hizo (BRT 3) yenye urefu wa kilometa 23.3 kuanzia katikati ya jiji la Dar es Salaam hadi Gongolamboto.

Akikagua ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo kwa haraka jana, Naibu Waziri Kasekenya alisema barabara hiyo ni lango la Jiji la Dar es Salaam na taifa kwa ujumla, hivyo serikali inategemea kuwa itakuwa barabara ya mfano kwa ubora na mwonekano.

"TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania) na mkandarasi hakikisheni barabara hii inajengwa kwa viwango vya kimataifa vya ubora na mwonekano. Licha ya kuwa lango kuu la kuingia nchini, pia ina historia ya kuitambulisha Tanzania kwa wageni," alisema.

Mhandisi Kasekenya alimtaka mkandarasi kuweka mfumo mzuri wa kudhibiti maji ya mvua ambayo yamekuwa kero kwa miaka mingi katika barabara hiyo na kuhakikisha yanaelekezwa kwenye mfumo mzuri ili kutosababisha mafuriko kwenye makazi ya watu.

Pia alisisitiza umuhimu wa mkandarasi kusimamia vizuri matumizi ya barabara wakati ujenzi ukiendelea ili watumiaji wa barabara wasipate adha na kusababisha msongamano na ajali zinazoweza kuepukika.

"Barabara unganishi zinazounga BRT na barabara zingine ziwe bora na salama wakati wote. Wekeni alama za barabarani wakati huu wa matengenezo," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Kasekenya aliwataka makandarasi watatu, wanaojenga BRT 4 kuongeza kasi ya ujenzi ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuondokana na msongamano wa magari.

Makandarasi hao ni kampuni za China Geo Engineering Corporation (CGC) anaeyojenga sehemu ya Maktaba Kuu ya Taifa – Morocco - Mwenge hadi Ubungo (kilometa 13.5), M/S Shandong Luquiao Group Co Ltd inayejonga barabara ya Mwenge hadi Tegeta Dawasa (kilometa 15.63) na China Communication Construction Co. Ltd inayojenga karakana ya mabasi hayo Kivukoni, Mbuyuni na Simu 2000.





# Bil. 870/- kukarabati vidakio vya maji

**Na Tumaini Mafie,**
ARUSHA

KIASI cha Sh. bilioni 870 kinatarajiwa kutumika kukarabati vidakio vya maji nchini baada ya kuharibiwa na shughuli za binadamu, imefahamika.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Mkurugenzi wa Bonde la Pangani, Segule Segule, wakati akizungumza katika mkutano wa wadau wa mipango ya uhifadhi wa vidakio hivyo nchini.

Segule, alisema kulingana na hali halisi iliyopo katika vidakio hivyo, bodi iliweka mikakati ya kudumu mojawapo ikiwa ni kupatikana fedha hizo kwa kipindi cha miaka 15 kwa ajili ya kukarabati.

"Kutokana na matatizo yaliyoainishwa kwenye vidakio, tumeweka makadirio ya Sh.bilioni 870, kwa ajili ya kukarabati vidakio vyote nchini, ambavyo jumla yake vipo tisa," alisema na kuongeza kuwa:

"Bodi ya Pangani pekee, inahitajika Sh.bilioni 180 ila kutokana na uharibifu mkubwa uliopo na kwa makadirio haya haimaanishi Bodi au Wizara ya Maji itatoa fedha hizi pekee, hapana tutashirikiana na wadau, wananchi na Bodi ya Maji."

Mkurugenzi huyo, alisema wanaamini jambo hilo litafanyika ndani ya miaka 15 ijayo ili vidakio hivyo viwe katika hali ya ubora zaidi.

Mgeni rasmi katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Taifa wa Jukwaa la Maji Mtambuka, Herbert Kashikilah, alitoa rai kwa wadau hao kuwa wabunifu katika kutatua matatizo yanayokabili mabonde ya maji ili kuhifadhi na kutunza mazingira.

Mkurungezi Msaidizi wa Rasilimali Maji wa Wizara ya Maji, Rosemary Rwebugisa, aliwataka wataalamu wa maji kufanya tathmini na kuchagua kidakio kimoja cha mfano.

Rosemary, alisema wizara hiyo itahakikisha inaweka nguvu ya pamoja kutunza kidakio hicho na kuhamasisha wadau kutunza vidakio vingine katika maeneo yao.

# WB yatoa mbinu kumaliza ufujaji ununuzi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKURUGENZI Mkazi wa Benki ya Dunia (WB) nchini, Nathan Belete amesema nchi za Afrika zinahitaji kutafakari kuhusu mifumo yake ya ununuzi na kuja na mifumo inayodhibiti ufujaji wa fedha za umma.

Belete alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa nne wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC) ulioandaliwa na Taasisi ya WAJIBU, ukishirikisha wataalamu kutoka mataifa mbalimbali.

"Suala hili haliwezi kushughulikiwa na wachache. Linapaswa kushughulikiwa kwa pamoja. Na nina furaha kwamba wote walio hapa, ni watu muhimu kwa sababu juhudi za pamoja zinahitajika ili kuleta mabadiliko na maendeleo katika nchi zetu husika," alisema.

Belete alisema kuwa nchi zinazoendelea zinakabiliwa na changamoto nyingi kama vile umaskini na mabadiliko ya tabianchi, suala ambalo linahitaji kutafutiwa ufumbuzi hasa wakati huu.

"Bara letu linahitaji mifumo madhubuti katika maeneo mbalimbali, ukiwamo ununuzi huku tukijitahidi kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, kwa sababu serikali duniani kote hutumia wastani wa Dola trilioni 9.5 katika kandarasi za umma kila mwaka na mikataba tu," alisema.

Alisema mikataba hiyo inalenga kuboresha maisha ya wananchi, hivyo ni wajibu wa kila mmoja wao kuhakikisha rasilimali hizo za umma zinachangia katika kuboresha maisha ya kila mtu.

Alisema WB inaendelea kujitolea kusaidia nchi wateja katika kubuni na kutekeleza programu za mageuzi ya ununuzi wenye lengo la kuongeza ufanisi na uadilifu na uendelevu wa mifumo ya ununuzi kupitia sheria thabiti za ununuzi.

"Tunafanya hivi kwanza kwa kutathmini ununuzi wa umma wa nchi husika, nguvu zake, udhaifu wake, kwa muda uliokubaliwa na hatua za kuboresha, tukitumia utaratibu maalum wa uhakiki wa mifumo.

"Benki ya Dunia inaandaa mikakati katika nchi mbalimbali wanachama ili kuimarisha mifumo ya ununuzi wa nchi. Kwa mfano, Benki ya Dunia ndiyo imekamilisha mikakati ya Tanzania Bara, mkazo maalum katika ufanisi wa ununuzi na ununuzi endelevu," alisema.

Balozi wa Sweden nchini, Charlotta Ozaki Macias, alisema katika kufikia uwiano wa uwazi na uwajibikaji, kunahitaji mbinu nyingi zinazojumuisha ukuaji uchumi, ushirikishwaji wa kijamii na ulinzi wa mazingira.

Balozi Macias alisema kipengele kimoja muhimu lakini kinapuuzwa mara nyingi ni mlinganisho katika ununuzi wa umma na kanuni za uwajibikaji na uwazi, ambazo ni tunu muhimu kupata maendeleo endelevu katika ulimwengu wa utandawazi.

Alisema mfumo mzuri wa ununuzi wa umma unaweza kuboresha jamii au kusaidia kuibua uzembe ili wananchi waiamini serikali yao huku akihimiza malipo kuambatanishwa na mahitaji ya uendelevu kwa kandarasi kupitia mifumo ya kielektroniki.

Alipongeza Tanzania kwa kupiga hatua kubwa katika ununuzi wa umma kwa kuimarisha mifumo ya kitaasisi, kujenga uwezo, kuboresha uratibu, mawasiliano, viwango, ufuatiliaji na tathmini na pia kukuza uwazi na uwajibikaji kwa kuhimiza ushiriki wa umma kuelewa ununuzi wa umma.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, alisema lengo la mkutano huo wa siku mbili ni kuwezesha wasimamizi wanaoshughulika na mifumo ya ununuzi, wawe na weledi na maadili katika kutekeleza miradi mbalimbali nchini.

Alisema serikali kuja na mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma (NeST) unaowezesha kushindanisha zabuni, hata kwa wajasiriamali wadogo, vijana, watu wenye ulemavu na wengine katika kuhakikisha miradi wanayoomba inaleta matokeo chanya katika kuchochea maendeleo kupitia TEHAMA.

"Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imekuja na mfumo huo mpya wa NeST unaowezesha sekta ya ununuzi kuboreshwa zaidi, hivyo shime Watanzania tumieni mfumo huu kwa ajili ya kupata zabuni mbalimbali," Utouh alisema.

Mkuu wa Uhusiano katika Ubalozi wa Norway nchini, Kjetil Schie, alisema ni muhimu wananchi kufuatilia ununuzi katika taasisi za serikali kuhakikisha kunakuwa na uwazi latika ununuzi wa umma.



Mkazi wa Kitongoji cha Mkababu, wilayani Handeni, mkoani Tanga, Maria Lekipa Laitayok, akiandaa chakula kwa kutumia nishati ya gesi jana, ikiwa ni sehemu ya mwitikio wa kampeni ya kumtua mama mzigo wa kuni kichwani iliyoasisiwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, iliyotambulishwa kitongojini hapo, miezi mitatu iliyopita. Kwa mujibu wa wakazi wa kitongoji hicho, kampeni hiyo imeleta ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya gesi ya kupikia badala ya mkaa na kuni kama ilivyokuwa awali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matumizi gesi safi yashika chati vijijini

**Na Mwandishi Wetu,**
HANDENI

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Tanga imeagiza kupunguza utoaji vibali vya ukataji miti ili kudhibiti matumizi ya mkaa na kuni kwa ajili ya kupikia na kuhamasisha matumizi ya gesi safi kwa wananchi hususani vijijini.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Albert Msando, baada ya kuwatembelea wakazi wa vijiji vya Msomera na Mkababu wilayani hapa kwa lengo la kufanya tathmini ya matumizi ya nishati hiyo na kubaini kuwa idadi kubwa ya wananchi wamepokea kwa mwitikio na kuanza kuachana na kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia majumbani.

Msando na viongozi wengine wa wilaya hiyo, walitembelea vijiji hivyo kwa ajili ya kufanya tathmini hiyo baada ya kuanzishwa kampeni ya kumtua mama mzigo wa kuni kichwani iliyoasisiwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

"Tuna imani ujio wa gesi hapa Handeni ni mwanzo mzuri kwetu na hatutarudi nyuma. Nimeagiza kupunguzwa kwa vibali vya ukataji wa miti inayotumika kuchoma mkaa kwa sababu sasa tuna lengo kuu la kupunguza matumizi ya kuni na mkaa katika wilaya hii," alisema na kuahidi yeye na viongozi wengine wilayani hapa kumuunga mkono Rais Samia ili kuhakikisha kampeni hiyo inafanikiwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakazi hao, walisema tangu kuanza kwa kampeni hiyo miezi mitatu iliyopita, wanawake wamejikita katika matumizi ya gesi na kukabiliana na changamoto ikiwamo za kimazingira na kiafya kwa kutumia mkaa na kuni kupikia.

Wanawake hao ni miongoni mwa wakazi 1,500 walionufaika na mitungi ya gesi kutoka kwa Kampuni ya Taifa Gas kwa kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Nishati, wamempongeza Rais Samia kwa kuanzisha kampeni hiyo na kunusuru afya zao.


Mmoja wa wakazi hao, Mariam Khatib, Mkazi wa Kata ya Chang'ombe, alisema nishati ya gesi inamwezesha kupika chakula haraka kwa ajili ya watoto wake ili waweze kuwahi kwenda shuleni.

Msimamizi wa Idara ya Mahusiano ya Umma katika kampuni hiyo, Angellah Bhoke, alisema fursa za kufungua maduka na vituo vya kujazia gesi katika programu hiyo ilitolewa kwa baadhi ya wakazi wa vijiji hivyo ili nao waweze kunufaika kiuchumi.

Kwa mujibu wa Bhoke, wanaendelea kufanya kazi na viongozi nchini wakiwamo mawaziri, wabunge, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na taasisi ili kufanikisha kampeni hiyo.

Kulingana na takwimu za kitaifa, takriban wananchi 33,000 hufa kila mwaka kutokana na athari za matumizi ya kuni na mkaa.

Vile vile, nchi inapoteza takriban heka 400,000 za misitu kila mwaka kutokana na matumizi haya. Hii ndiyo chanzo cha kampeni ya matumizi ya nishati safi nchini kama ilivyozinduliwa na serikali.





# Wenje ajitosa kinyang'anyiro Makamu M'kiti CHADEMA

**Na Remmy Moka,** SAUT

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Victoria, Ezekiah Wenje, ametangaza nia ya kugombea nafasi ya makamu mwenyekiti wa chama hicho taifa katika uchaguzi utakaofanyika hivi karibuni.

Wenje ametangaza nia hiyo juzi jijini Mwanza wakati akizungumza na wanachama wa CHADEMA wa kanda hiyo, akisema chama hicho ni cha kidemokrasia, hivyo ni ruksa kwa kila mwanachama kugombea nafasi yoyote.

Alisema ametangaza nia yake hiyo kwa kuwa ana uwezo wa kukiongoza chama hicho katika wadhifa huo ngazi ya taifa.

Wenje ambaye alichaguliwa kuiongoza kanda hiyo hivi karibuni, pamoja na mambo mengine alisema lengo la CHADEMA ni kushika dola nchini na kusuluhisha matatizo yanayowakabili wananchi, na ndiyo sababu inayompa msukumo wa kuwania nafasi hiyo ya juu kitaifa mara chama hicho kitakapopuliza kipyenga.

Alitaja baadhi ya matatizo hayo kuwa ni ubovu wa miundombinu, ukosefu wa ajira na kuinua sekta muhimu kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi.

Kwa upande mwingine, Wenje alitumia mkutano huo kuiomba serikali kuweka mifumo rafiki ya elimu bunifu kwa wanafunzi ili kukabiliana na changamoto za maisha na kuanzisha mitaala ya kujifunza kwa vitendo.

Vilevile, alishauri kuwekeza zaidi katika kilimo cha kisasa na kutoa elimu kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji wa chakula nchini na kukuza mitaji yao.

Akizungumzia kuhusu utafiti, Wenje aliishauri serikali kuongeza ushirikiano na taasisi za kimataifa ili kupata ujuzi zaidi na rasilimali kwa kubadilishana taaluma na wataalamu.

Alikumbusha kuweka soko la pamoja katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kusaidia kukuza mzunguko wa biashara na kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara kuendelea kutegemea soko la Kariakoo lililopo jijini Dar es Salaam kukuza uchumi wao.

Kuhusu uchaguzi mkuu mwakani pamoja na wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu, Wenje aliitaka serikali kuweka mifumo rafiki katika chaguzi hizo, kuondoa ubadhirifu wa fedha, kuleta tija kwa kuufanya kuwa huru na wa haki kwa vyama vyote vya siasa nchini.



Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu Prof. Mussa Assad (wa pili kulia), akikata utepe kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Hospitali ya Kiislamu Mkoa wa Tanga, katika Kata ya Masiwani jijini Tanga juzi. Kulia ni Sheikh wa Mkoa huo, Juma Luwuchu na wa pili kushoto ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Sheikh Khamis Mataka. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Kiongozi wa mtaa arejesha michango ya wananchi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWENYEKITI wa Mtaa wa Kagongwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Michael Shija, amerejesha Sh. milioni 7.452 zilizochangwa na wananchi kununua eneo la maziko na kubatilisha matumizi kwa kujenga matundu 10 ya choo katika Shule ya Msingi Kanegere bila ya kuwashirikisha.

Fedha hiyo zilikabidhiwa juzi na Diwani wa Kata ya Kagongwa, Ismail Masolwa katika mkutano wa hadhara uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa na Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba.

Masolwa, alisema fedha hizo zilichangwa na wakazi wa mtaa huo mwaka jana baada ya kukubaliana kununua eneo la maziko badala yake, Mwenyekiti Shija alibatisha matumizi yake bila vikao na kujenga matundu 10 ya vyoo hali iliyosababisha wananchi kudai.

Masolwa, alisema fedha hizo zitarejeshwa kwa wananchi kupitia umoja wao wa kusaidiana (Nzengo) na kuangalia namna ya kuelekeza kwenye shughuli nyingine za maendeleo.

Alisema eneo la maziko ambalo lilitakiwa kununuliwa limepatikana na kuwataka wakazi hao kuendelea kuwa na moyo wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Mkazi wa mtaa huo, Masanja Nzingula, alisema walikerwa na kitendo cha fedha hizo kubatilishwa matumizi kwa kuelekezwa kwenye ujenzi wa vyoo vya shule bila kushirikishwa.

Nzingula, aliwataka viongozi wengine kuacha tabia hiyo kwa kuwa inaweza kusababisha wananchi kuvunjika moyo kujitokeza kuchangia maendeleo katika maeneo yao.

Mbunge Kishimba, alisema alikuwa akilalamikiwa na wakazi wa mtaa huo kuhusiana na fedha hizo.

Alisema katika mkutano wa hadhara Machi 16, mwaka huu, mwenyekiti huyo aliahidi kurejesha fedha hizo, hivyo kuondoa malalamiko hayo baada ya kukabidhi.

Kishimba aliwataka viongozi wa vijiji, mitaa na kata kuacha tabia ya kushika fedha zinazotolewa na wananchi na badala yake zipitie benki na kama kutakuwa na mabadiliko ya matumizi ya kile kilichokusudiwa washirikishwe na kuamua.

## Madiwani waja juu ubovu barabara

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, wamekuja juu na kutaka barabara zilizoharibiwa na mvua zifanyiwe matengenezo ya haraka ili kuondoa kero kwa wananchi.

Wakizungumza kwenye kikao cha baraza la madiwani la halmashauri hiyo cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2023/2024, walisema kutopitika kwa barabara hizo kutokana na mashimo ni kikwazo katika shughuli za uchumi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Wiliam Jijimya, alisema ubovu wa barabara katika maeneo yao, limekuwa tatizo kubwa na kumtaka Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kuzifanyia ukarabati mara moja.

"Miundombinu ya barabara hapa wilayani Kishapu ni mibovu na nyingine hazipitiki kabisa sababu ya kuharibiwa na mvua, zifanyiwe matengenezo," alisema Jijimya.

Kaimu Meneja wa TARURA wa Halmashauri hiyo, Joseph Bahati, alisema wapo kwenye mpango wa kukarabati barabara hizo.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, aliitaka TARURA kuwapa kazi za kukarabati barabara hizo makandarasi wenye uwezo na kukamilika kwa wakati.

## Wakulima wa pamba wapewa somo

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAKULIMA wa pamba wameshauriwa kutumia kwa usahihi mbolea ya asili iliyoongezwa virutubisho kwa maandalizi ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo na uchumi.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Ofisa Kilimo wa Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Penina Lange, katika Maonesho ya Nanenane Kanda ya Ziwa Magharibi yanayoendelea katika viwanja vya Nyamhongolo mkoani Mwanza wakati akitoa elimu ya kilimo bora cha pamba kwa wakulima.

"Tunawahimiza wakulima kutumia mbolea hai ambayo inapatikana katika mazingira yanayowazunguka kama maji, kinyesi cha ng'ombe kibichi na majivu ambayo kwa pamoja wakichanganya na viuatilifu vingine inasaidia," alisema Lange.

Mtaalamu wa Kilimo cha Pamba, Renatus Ruziba, alisema teknolojia hiyo imeanza kuleta matokeo kwa wakulima.

Akizungumza katika banda hilo, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hasani Masala aliitaka bodi hiyo kuongeza nguvu katika utoaji wa elimu kwa wakulima ili kuinua kilimo hicho na uchumi wao.

"Kanda ya Ziwa ni wadau wakubwa wa pamba endeleeni kuwaelimisha namna ya kutumia teknolojia ili lizidi kuwa zao la biashara katika mikoa yetu," alisema Masala..



Ukurasa 12

**Udanganyifu kuboresha daftari unavyoweza kukutupa gerezani**



Ukurasa 13

Viongozi wapya TLP wanapomsihi msajili kunasua mkwamo haraka


siasa

JUMATANO AGOSTI 7, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**UCHAGUZI AMERIKA**

**Trump adaiwa kuelekea 'kuomba poo,' akipokonywa ajenda kuu ya kampeni**

# Wanawake wapiganaji wanavyosimamia mageuzi kiutendaji tasnia ya habari - 2

**Na Jenifer Gilla**

***WIKI iliyopita ilichapisha sehemu ya kwanza ya makala hii inayohusu mapinduzi ndani ya vyombo vya habari yanayofanywa na wanahabari wanawake viongozi.***

Itakumbukwa kuwa miaka ya 1980 vyombo vya habari nchini viliongozwa na wanaume na kuathiri utendaji kazi wa wanawake ndani ya taasisi hizo na maudhui yaliyochapishwa.

Leo zama zimebadilika, wanawake viongozi walioko kwenye harakati za kuleta usawa wa kijinsia ndani ya vyumba vya habari, wanabadilisha mambo kama anavyoeleza Mhariri Mwandamizi Kitengo cha Maundhui Mitandaoni, Azam Media, Jennifer Sumi.

"Nilipitia changamoto zinazofanana na wahariri wengi akiwamo Beatrice Bandawe, kubwa likiwa ni kudharauliwa na baadhi ya niliokuwa nawasimamia wakiamini kuwa hawapaswi kupangiwa majukumu na mwanamke." Anasema .

Anafafanua kuwa hali hiyo ilimlazimu kutumia busara na urafiki kama kiongozi badala ya ubabe mpaka pale watu hao walipokubali kuwa ndiye kiongozi wao na hawana jinsi nyingine zaidi ya kumpokea.

**MABADILIKO WALIOLETA**

Baada ya uteuzi wa Beatrice Bandawe, kuwa Mhariri Mtendaji wa Nipashe, anasema aliona haja ya kurekebisha baadhi ya mambo aliyodhani yanazorotesha utendaji.

Anasema ni pamoja na kubadilisha mrengo wa uandishi wa habari kwa kuweka ujumuishi wa makundi mbalimbali kama vile wanawake, watoto na wanaoishi na ulemavu.

"Tulijiwekea mikakati kuwa sauti za makundi mbalimbali ya wanawake, wazee, vijana, na wenye ulemavu zinakuwapo ili matatizo yao yasikike na yatolewe ufafanuzi au kusuluhishwa" anasema.

Beatrice anayeshikilia nafasi hiyo kwa miaka mitano sasa pia aliondoa mgawanyo uliokuwapo baina ya wafanyakazi na kuwaweka pamoja, hali iliyosaidia wote walio chini yake kufanya kazi kwa kushirikiana na kuwapunguzia mzigo wahariri wakati wanapitia na kuhariri habari.

Anaongeza kuwa anajivunia kubadilisha mawazo ya waandishi wengi walioamini kuwa nafasi za uongozi ni za wanaume pekee.

"Mwanzoni ilikuwa kazi fulani inaonekana ya kufanya wanawake na nyingine wanaume, lakini katika uongozi wangu kila mtu ni sawa, kwa hiyo hata ugawaji wa majukumu ninahakikisha unaenda kwa usawa," anasema.

Jennifer Sumi Mhariri Mwandamizi Kitengo cha Maundhui Mitandaoni, Azam Media, anaeleza kuwa pamoja na changamoto alizopitia bidii na uaminifu mkubwa kwenye kazi vilibadilisha mtazamo kuwa mwanamke hawezi.

"Ulibadilika hadi ukawa wanawake ndiyo wanaweza zaidi katika kitengo cha maudhui mtandaoni."

Anajivunia mapinduzi aliyofanya katika kitengo cha kidijitali kwa miaka saba mpaka sasa ndani ya chombo hicho, akisema ni miongoni mwa vinavyofuatiliwa na kuaminika mitandaoni na hata ile ya kijamii.

Anataja siri kuwa ni kujifunza vitu vipya ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia:

"Nimeshiriki kozi nyingi za masuala ya maudhui ya mitandaoni na dijitali, akili mnemba, habari za uzushi, kutengeneza video za kurusha mitandaoni mpaka na ninaendelea na mafunzo."



Mwenyekiti wa TAMWA, Rose Ruben.

Joyce Shebe kutoka Clouds Media anajivunia kubadilisha mitazamo kwa baadhi ya watu waliokuwa wanadhani mwanamke hawezi kushika wadhifa wa juu na kuongeza tija ya umuhimu wa kushirikisha sauti za wanawake na wanaume katika maudhui yanayoandaliwa. Anasema pia amebadilisha dhana iliyokuwa imejengeka katika ofisi yake kuwa baadhi ya majukumu kama vile kupiga picha, kuchukua video, kuchanganya sauti ni ya wanaume huku wanawake wakijikita zaidi kwenye utangazaji na kuandika.

Anasema amesisitiza kila mwandishi kujua majukumu yote kwenye uandishi wa runinga na kuwa mahiri. Anasema mabadiliko hayo yalifanya Clouds Media Group kuwa bora kwenye kutoa maudhui na baadhi ya ripoti zilizofanyika zilionyesha chombo hicho hutoa maudhui yanayozingatia usawa wa kijinsia.

Joyce pia amefanikiwa kutengeneza sera ya jinsia katika chumba cha habari kwa kushirikiana na TAMWA ambayo imeondoa unyanyasaji wa kijinsia katika eneo lao la kazi.

Mwandishi wa habari wa Clouds Media, Sophia Kessy anatoa ushuhuda wa mabadiliko ya kiutendaji yaliyoletwa na kiongozi Joyce, akisema amekuwa akiwahimiza waandishi kuendelea kujifunza mbalimbali ya kiuandishi na kuwaunganisha katika fursa hiyo ili wakuze taaluma zao.

Anasema pia amepata motisha kuwa atafanya kazi kwa bidii siku moja atakuwa kiongozi katika chumba cha habari.

Anaeleza kuwa hapo awali hakuwahi kudhani kuwa mwanamke anaweza kuongoza vyumba vya habari kutokana na dhana iliyojengeka kuwa mwanaume pekee ndiyo mwenye uwezo huo.

Mwandishi Beatrice Shayo wa Nipashe, anasema kupitia viongozi wanawake kwenye vyombo vya habari amejifunza kuwa elimu ndiyo msingi wa kujiamini na kuzifikia ndoto hivyo amerudi shule ili kuboresha ufanisi.

**KWANINI WALICHAGULIWA**

Mhariri Mtendaji wa gazeti la Mwananchi, Joseph Damas, anasema viongozi wanawake katika vyombo vya habari wameonyesha uwezo katika utekelezaji wa majukumu yao na hawakupewa nafasi kwa upendeleo.

INAENDELEA UK. 13

# Udanganyifu kuboresha daftari unavyoweza kukutupa gerezani



Mkazi wa Karyambwa mkoani Kagera, Vedastus Manyansinde, akiboresha taarifa zake katika Daftari la Kudumu la Wapigakura, katika kituo cha Shule ya Msingi Rubungo. **PICHA: MROKI MROKI**

**Na Mroki Mroki, INEC**

Ibara ya 74(6) (a) na (d) ya Katiba ya Tanzania, inaipa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), jukumu la kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapigakura katika uchaguzi wa rais na wabunge wa Bara na Visiwani na ule wa madiwani kwa Tanzania Bara.

Wakati Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), inasimamia uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, wajumbe wa baraza la wawakilishi na masheha wa sheria za visiwani humo.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 16(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024, INEC ina wajibu wa kuboresha daftari la kudumu la wapigakura mara mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja uliomalizika na kabla ya tarehe ya uteuzi wa wagombea kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaofuata.

Katika kutimiza matakwa hayo ya kikatiba na kisheria Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeanza kuboresha daftari hilo ambapo uzinduzi ulifanyika mkoani Kigoma Julai 20 mwaka huu, mgeni rasmi akiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Uzinduzi huo ulikwenda sambamba na kuanza kwa mzunguko wa kwanza wa uboreshaji kwenye mikoa mitatu ya Kigoma, Tabora na Katavi na mzunguko wa pili umeanza Jumatatu Agosti 05 hadi 11, 2024 kwa mikoa ya Geita na Kagera.

> Tume inatekeleza jukumu lake hili la kuboresha daftari la kudumu la wapigakura kwa mujibu wa katiba na sheria iliyotungwa na bunge.

Ikumbukwe kuwa mara ya mwisho Tume iliboresha daftari mwaka 2019/2020, hivyo, ina wajibu wa kuboresha mara mbili kabla ya tarehe ya uteuzi wa wagombea kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwakani.

Mengi yalizungumzwa na Waziri Mkuu Majaliwa wakati wa uzinduzi huo pale Kigoma ambapo kubwa alisisitiza uzalendo wakati wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura.

Aidha, alisema kuwa kila Mtanzania ashiriki katika usimamizi wa suala hilo kwani wanaotakiwa kuandikishwa ni raia wa Tanzania tu wenye sifa zilizobainishwa kwa mujibu wa sheria.

"Wananchi ni watambuzi wa kwanza, niwasihi sana tuwe wazalendo, huu ni wajibu wa raia wa Tanzania kuhakikisha wanaoandikishwa ni Watanzania tu," anasema katika sehemu ya hotuba yake.

Lakini uzalendo una maana pana na moja ya sifa ya mzalendo ni yule anayefuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na taifa lake ili serikali au mamlaka husika iweze kuongoza.

Tume inatekeleza jukumu lake hili la kuboresha daftari la kudumu la wapigakura kwa mujibu wa katiba na sheria iliyotungwa na bunge. Wapo wananchi ambao wameamua kujitoa uzalendo na kuamua kuvunja sheria halali zilizotungwa na bunge.

Hawa si wengine bali ni wale wanaojiandikisha zaidi ya mara moja ilhali wakijua kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Ndio ni kosa, ukisoma kifungu cha 114(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024 kinaeleza wazi kuwa kujiandikisha zaidi ya mara moja ni kosa ambalo linaweza kukupelekea ukatumikia adhabu ambayo ukitiwa hatiani unaweza kulipa faini isiyopungua Sh.100,000 na isiyozidi shilingi 300,000 au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Uongo ni jambo lingine ambalo litakupelekea kuingia matatizoni maana wapo wananchi ambao hufanya udanganyifu wakati huu wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura.

Hawa ni wale ambao wanatoa taarifa za uongo kwa ofisa mwandikishaji au kutoka kwa mtu mwingine yeyote ambaye ana wajibu juu ya maombi ya kuandikishwa au kutoa kadi ya mpigakura, atatoa taarifa yoyote ya uongo kuhusu ombi lake mwenyewe au kwa niaba ya mtu mwingine kuandikishwa au kupewa kadi ya mpigakura, kufanya hayo ni kosa kisheria.

Aidha, kuna wale ambao waliendа kuandikishwa katika eneo la uchaguzi wakati wameshaomba kuandikishwa katika eneo lingine la uchaguzi na maombi yake ya awali hayajaamuliwa kwa kusubiri uchunguzi wowote kuhusu sifa za mwombaji au kuondolewa, hili nalo ni kosa.

Makosa mengine yanayotajwa katika kifungu cha 114(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024 ni pamoja na kuiba, kuuza, kununua kadi ya mpigakura kutoka kwa mtu mwingine ili aonekane kuwa ni mpigakura aliyeandikishwa kihalali na kuharibu kadi ya mpigakura.

Hivyo ni vyema kuepuka makosa hayo ili kujiepusha na adhabu za faini na kifungo.

Pia ni muhimu ikakumbukwa kuwa wale wote ambao hapo awali walishajiandikisha na kadi zao za mpigakura zipo vizuri kwa maana hazijaharibika na hazijapotea hawana haja tena ya kujitokeza kwenda vituoni kujiandikisha kwani kadi walizonazo ni halali kwa mujibu wa sheria.

Julai 25, 2024, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele, wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Geita alitoa ufafanuzi wa kina juu ya wanaojitokeza kujiandikisha zaidi ya mara moja.

Jaji Mwambegele alisisitiza kuwa hakuna uwezekano wa mtu kujiandikisha mara mbili na taarifa zake kusalia kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa kuwa kabla ya kutoa nakala ya mwisho, tume hulisafisha daftari kwa kuwaondoa wapigakura waliojiandikisha zaidi ya mara moja.

"Baada ya uandikishwaji wa wapiga kura kukamilishwa, taarifa zote huingizwa kwenye mfumo wa AFIS (Automated Finger Print Identification System) ambao huwaonesha wote waliojiandikisha kwenye daftari zaidi ya mara moja. Wapigakura wa aina hii hufutwa moja kwa moja kwenye vituo vyote na kuwabakisha kwenye kituo alichojiandikisha mara ya mwisho," anasema Jaji Mwambegele.

Orodha ya watakaojiandikisha zaidi ya mara moja itapelekwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya hatua za kisheria na kwamba tume imekua ikifanya hivyo katika chaguzi za nyuma ambapo katika uandikishaji uliofanyika 2015, INEC ilibaini jumla ya wapiga kura 52,078 waliojiandikisha zaidi ya mara moja na walichukuliwa hatua za kisheria.

Wakati wa kuboresha daftari wa mwaka 2020, tume ilibaini majina ya watu 42,301 ambao walijiandikisha zaidi ya mara moja na orodha hiyo ilikabidhiwa kwa vyombo vinavyohusika na makosa ya kijinai.

Baada ya kukamilika kwa uchakataji wa daftari, tume huchapisha na kuweka wazi daftari hilo chini ya kifungu cha 24 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ambapo wananchi hulikagua.

Kumbuka "Kujiandikisha kuwa mpigakura ni msingi wa uchaguzi bora" na hiyo ndiyo kauli mbiu ya uboreshaji wa mwaka huu.

# Viongozi wapya TLP wanapomsihi msajili kunasua mkwamo haraka

**Na Sabato Kasika**

UMETIMIA mwezi na siku nane sasa, tangu Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), kifanye uchaguzi wa mwenyekiti taifa, lakini ukakataliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ikisema hautambui.

Mwenyekiti wa TLP Taifa, alichaguliwa Juni 29, mwaka huu ni Aivan Maganza, kutangazwa rasmi kushika wadhifa huo, uliokuwa unashikiliwa na Augustine Mrema aliyefiriki dunia mwaka 2022.

Hata hivyo, hadi sasa hajaingia ofisini kufanya kazi, kutokana na kile kinachoelezwa kuwa ni kuzuiliwa na walinzi wa makao makuu ya chama hicho, yaliko Magomeni Usalama Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam wiki hii Maganza anasema, taarifa za kuzuiwa kwake kuingia ofisini, zipo kwa Msajili wa Vyama vya Siasa na kwamba hadi sasa hakuna hatua zilizochukuliwa.

"Tulifikisha malalamiko yetu ofisini kwake baada ya Richard Lyimo aliyekuwa katibu wa chama kuweka mabaunsa wa kutuzuia kuingia ofisini, tukaahidiwa kuwa suala hili lingeshughulikiwa haraka, lakini ajabu ni kwamba hadi leo ni kimya," analalamika Maganza.

Anafafanua kuwa , anaumia anapoona ofisi ya chama inachezewa na mtu ambaye pengine hana mamlaka ya kufanya hivyo, na kwamba hali hiyo ikiendelea watalazimika kuchukua maamuzi mengine.

Mwenyekiti huyo mpya anataja maamuzi hayo ni kwenda mahakamani ili suala la mgogoro wao lishughulikiwe na mahakama iwapo wataona ofisi ya msajili inaendelea kuwa kimya.

"Lyimo alikuwa katibu mkuu lakini, baada ya uchaguzi, halmshauri kuu ya chama ilimvua nafasi hiyo na kubaki mwanachama wa kawaida, hata hivyo, inasikitisha kuona anakuwa na nguvu kiasi hicho?" Anahoji.

## • Wakili ataka migogoro iundiwe chombo huru



Mwenyekiti mpya wa TLP, Aivan Maganza alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kuchaguliwa. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti, Dominatha Rwechungura. **NA MPIGAPICHA WETU**

Anasema, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilikuwa imeahidi kumaliza sintofahamu hiyo ya kiongozi Julai 17 mwaka, na kwamba tangu ahadi hiyo itolewe, hakuna ambacho kimefanyika.

Maganza anasema, anaumia anapoona chama kinakwama kufanya kazi kutokana na watu wachache wanaong'ang'ania madaraka na kusababisha kishindwe kujiandaa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Chama ni wanachama, bila wanachama hakuna chama. Tumefanya uchaguzi ili tujipange upya kurudisha wanachama na kutafuta wengine wapya wa kutuunga mkono, lakini pia kujipanga kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani, lakini tunazuiwa kuingia ofisini na mtu anayeng'ang'ania madaraka," anasema.

Anasema, TLP inaihimiza Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuharakisha kumaliza mgogoro huo ili yeye na timu yake waingie ofisini watekeleza majukumu yao kurudisha uhai wa chama hicho.

### JICHO KWA MSAJILI

Akizungumzia migogoro ndani ya vyama, ambayo haijapata ufumbuzi wa msajili ikiwamo wa NCCR -Mageuzi na sasa TLP, wakili Jebra Kambole, anasema, kinachochangia migogoro hiyo, ni Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutokuwa huru na pia kukosekana ukomo wa kusikiliza migogoro.

"Huu ni mtazamo wangu kwamba, ofisi hiyo haiko huru, inafanya kazi kwa namna ambavyo bajeti yake inapatikana, lakini pia haina ukomo wa kusikiliza migogoro ya vyama, hicho ndicho chanzo cha yote yanayoendelea," anasema Kambole.

Ili kumaliza hayo, anashauri kiundwa chombo kingine huru cha kuisikiliza.

"Linaweza kuundwa baraza la usuluhishi wa migogoro ya kisiasa litakalokuwa chini ya msajili na wajumbe wachache, akiwamo kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kutoka Chama cha Wanasheria wa Tanganyika -TLS, wabobezi wa siasa, vyama vya upinzani, taasisi za kidini, asasi za kiraia na vyombo vya habari," anasema.

Anaamini, hayo yakifanyika, migogoro ya vyama inaweza kuisha, kwa kuwa baraza litaendesha shughuli zake kwa uhuru kuliko ilivyo sasa, na kwamba migogoro inayokwama ndani ya ofisi ya msajili imekuwa ikififisha nguvu za vyama vya upinzani.

Wakili huyo anasema kuondoa migogoro ndani ya vyama vya siasa ni sawa na kuimarisha demokrasia kuharakisha maendeleo na vyama husika, ili navyo viwe na mchango kwa maslahi mapana ya nchi.

### KAULI YA MSAJILI

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, akizungumza na gazeti hili jana, anasema ahadi ya kutatua mgogoro huo ipo palepale, kwa kuwa tayari umefika ofisini kwake.

"Tunaendelea kulifanyia kazi tatizo la TLP, hivyo wanaolalamika wavumilie, kwani ofisi inafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu, si kwa matakwa ya mtu fulani," anasema Nyahoza.

Anafafanua kuwa walipata kufanya maamuzi Julai 17 mwaka huu, lakini haikuwa hivyo, kwa maelezo kwamba bado hawajamaliza kupitia kwa kina malalamiko ya pande mbili zinazolumbana.

"Niwaombe waendelee kuwa na subira tukimaliza kupitia maelezo ya pande zote tutatoa majibu. Ikumbukwe kuwa chama kikichagua kiongozi wa juu, lazima ofisi ya msajili ipitie hatua kwa hatua fomu za maelezo ya uchaguzi ulivyofanyika, ijiridhishe ndipo itoe maelekezo," anasema.

Anasema, ofisi yake ilipokea taarifa ya uchaguzi huo kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa TLP Taifa, Dominatha Rwechungura, kisha ikamwagiza Lyimo kutoa maelezo kwa nini anapinga uchaguzi huo.

"Kwa hiyo hayo yote tunayapitia kwa umakini hasa baada ya Lyimo kuiambia ofisi hiyo kuwa hakuwa na taarifa yoyote kuhusu chama kufanya uchaguzi uliompa ushindi Maganza.

## Wanawake wapiganaji wanavyosimamia mageuzi kiutendaji tasnia ya habari-2

**INATOKA UK. 11**

Anatoa mfano katika idara yake ana viongozi wanawake wawili na mwanamume mmoja na ni kwa sababu walionyesha utayari wa kujifunza mambo mapya na hata alipowachagua kushika nafasi hizo wanafanya kazi kwa bidii.

### WANAVYOPIKWA

Mratibu wa Mradi wa Mafunzo ya Uongozi kwa Waandishi wa Habari Wanawake, Unaotekelezwa na Shirika la Kimataifa la WAN-INFRA/Women in News, Dk. Joyce Bazira, anasema tangu mwaka 2015 wamekuwa wakiwapika waandishi wa habari wanawake nchini kushika nafasi za juu za uongozi katika vyombo vya habari, jambo linalofanikiwa uwakilishi huo.

Dk. Joyce anasema mpaka sasa shirika hilo limetoa mafunzo kwa waandishi wa habari 75 nchini, wengi wao wameonyesha mabadiliko makubwa kwenye utendaji kazi, michango yao kuonekana katika tasnia na kualikwa sehemu mbalimbali na kupata nafasi za juu za uongozi.

"Mfano ni Beatrice Bandawe, wakati anapata mafunzo haya alikuwa ni mwandishi wa kawaida, lakini tumeendelea kumpa mafunzo ya mara kwa mara ya kumjengea uwezo na ameyafanyia kazi mpaka sasa hivi amekuwa ni Mhariri Mtendaji," anasema.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, anasema uwepo wa viongozi wanawake katika vyombo vya habari imefanikisha kupunguza vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ambao ulikuwa unasababishwa na viongozi wa kiume.

Anasema hapo awali wanaume walikuwa wakitumia mwanya kuwa katika nafasi za juu kuwanyanyasa wanawake kwa kupenyeza unyanyasaji kingono.

Aidha, walipokataa waliwajengea mazingira ya kuonekana hawafai kazini, jambo ambalo kwa sasa limepungua kwa sababu wanawake wanashika nafasi hizo.

Aidha, imeongeza sauti za wanawake katika maudhui ya habari kwa sababu wanawake wamekuwa wakifuatilia na kuhakikisha sauti zao na za makundi mengine zinakuwapo hali inayochangia usawa wa kijinsia katika makala hizo.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, anasema kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na serikali wanaendelea na jitihada kuhakikisha kuwa vyombo vya habari vinakuwa maeneo salama ya kazi kwa wanawake na wanaume.

JUKWAA LA VIONGOZI

UCHAGUZI AMERIKA

# Trump adaiwa kuelekea 'kuomba poo,' akipokonywa ajenda kuu ya kampeni

• Ilikuwa Biden ni mzee, mgonjwa tena wa maradhi ya usahaulifu

Na Gaudensia Mngumi



Mgombea urais wa Marekani, Makamu wa Rais, Kamala Harris.

YULE mbabe Donald Trump, aliyeiita Afrika shimo la kinyesi cha binadamu, lakini akawatukana Waafrika kuwa wanastahili kutawaliwa na wakoloni kwa karne nyingi zaidi, anapata wakati mgumu kwenye uchaguzi wa Marekani, unaoshika kasi mpya.

'Babu' (78), huyo aliyesema Waafrika mbali na kupenda ngono na uvivu hawana sifa nyingine, anaendelea kugaragazwa na mpinzani wake Makamu wa Rais Kamala Harris, na inavyoelekea 'ataomba poo'.

Makamu wa Rais Kamala Harris (58), amepunguza uongozi wa Rais wa zamani Donald Trump tangu achukue kampeni za urais kutoka kwa Joe Biden, kulingana na kura nyingi anazopata sasa.

Uchunguzi wa hivi karibuni wa Morning Consult, unamwonyesha Kamala akiongoza kwa pointi nne mbele ya Trump, ambayo ni rekodi ya juu kwa urais wa mgombea wa Democrat katika miaka ya hivi karibuni, kwa mujibu wa taarifa za Jarida la Forbes la Marekani la Jumatatu wiki hii.

Forbes inasema Kamala anaongoza dhidi ya Trump kwa asilimia 48 dhidi ya 44 katika kura za hivi punde zaidi ya Morning Consult iliyotolewa Jumatatu, huku asilimia tano ya wapigakura waliojiandikisha waliohojiwa wakichagua "mtu mwingine" na siyo Trump.

Jarida, linaongeza kuwa wiki ya tatu mfululizo kura ya maoni ya kila wiki ya Morning Consult imeonyesha hayo.

Mambo ambayo hayakutarajiwa yamebadilisha upepo wa uchaguzi wa Marekani baada ya kuteuliwa Kamala kama mbadala wa Biden, na kuuingiza uchaguzi huo katika sura ya kuking'arisha chama tawala cha Democrat.

Itakumbukwa kuwa uteuzi wa Makamu wa Rais Kamala wa Democrat umeongeza kasi mpya katika kinyang'anyiro hicho, licha ya kwamba kutakuwa na athari kadhaa kwa uchaguzi na mitizamo ya Waamerika.

Kugombea kwake kunaweza kuzidisha mgawanyiko ulio tayari nchini humo kati ya mikondo miwili inayopingana mmoja, unaowakilishwa na Wanademokrat ambao wanaambatana na sheria zilizopo za mfumo wa kisiasa wa Marekani wanaoina nchi hiyo kuwa chungu cha wahamiaji kutoka popote duniani.

Mkondo mwingine ni ule unaowakilishwa na Donald Trump na Republican, ambayo inatilia shaka uhalali wa mfumo huo na taasisi zake na kuwaona wahamiaji kama sababu kuu ya shida na changamoto zinazoitesa Amerika leo.

Kuinuka ghafla kwa Kamala kwenye uteuzi huo, kufuatia matokeo duni ya mdahalo wa Rais Biden yaliyomfanya ajiondoe kwenye kinyang'anyiro cha urais, kumebadilisha uchaguzi na kupelekea Wanademocrat kukiunganisha chama na kuongeza imani katika nafasi zake za ushindi.

> Wakati huu, msukosuko unaweza kuwa mbaya zaidi. Trump anapoendelea kudai kuwa hana imani na taasisi za serikali na kusisitiza kuzisafisha, iwapo atashinda.

Siku moja baada ya kutangazwa kugombea kwake, Kamala aliuungwa mkono na wajumbe 1,976 wa Democrat, kiasi cha kutwaa uteuzi wa chama katika kongamano lake.

Ndani ya siku chache, kampeni ya Makamu wa Rais ilivunja rekodi ikipata Dola milioni 231 za michango ya kampeni, hasa kutoka kwa wafadhili wadogo na bado vigogo wazito.

Mabadiliko hayo yameonekana katika idadi ya wapigakura na nyingi sasa zinampa uongozi wa kinyang'anyiro hicho kwa pointi nne dhidi ya Trump, ambaye mwezi Juni alikuwa akichuana na Biden kwa ulinganifu.

Takwimu za karibuni zinaonyesha kuwa huenda kuna kurejea kwa majimbo mbalimbali ya Democrat ambayo yalikuwa yamemwacha Biden kutokana na kuunga mkono shambulio la Israel huko Gaza, ikijumuisha sehemu muhimu za tawi la vijana la chama hicho na wapigakura Weusi na Waislamu.

Wakati Kamala bado hajapata tena uungwaji mkono kamili wa vikundi vilivyochangia ushindi wa Rais Biden mwaka 2020, historia yake ya mapambano, na ukweli kwamba hajahusishwa moja kwa moja na msimamo wa Biden kwenye vita vya Israeli, vimewavutia wengi wa wapiga kura.

Biden kumwidhinisha Kamala kuwa mgombea pia kutaongeza kuungwa mkono kati ya wafanyikazi na wapigakura wa chama hicho waliomuunga mkono Biden katika uchaguzi uliopita.

## KUPORWA AGENDA

Uteuzi wa Kamala umeupokonya upande wa Trump agenda muhimu ya kura na mkakati wake wa kampeni kwamba Biden ni mzee, mgonjwa, tena anaumwa maradhi ya kukosa kumbukumbu.

Mkakati huo ulilenga kuelezea upungufu wa Biden, uwezo wake wa kiakili na uongozi na madai ya ufisadi yanayomhusisha mtoto wake.

Japo mabadiliko haya hayamhakikishii ushindi Kamala lakini yamebadilisha mienendo ya uchaguzi. Uwepo wa Biden ulianza kuwakatisha tamaa wapigakura wake, wakati chama cha Republican kilikuwa kimejipanga, kujiamini na kuwekeza kikamilifu kwa mgombea wake Babu Trump, hivyo ujio wa Kamala unabadili mlinganyo huo.

## TRUMP KAMA AFRIKA

Ni mazoea kwa wapinzani wa Afrika kulalamika kura kuibwa, kubadili matokeo na serikali kuingilia uchaguzi, ndicho anachofanya Trump sasa.

Trump ana wasiwasi kuwa kuna uwezekano wa uchaguzi mkali jambo linaloweza kusababisha machafuko yaliyotokea baada ya uchaguzi wa 2020, wakati Trump alikataa matokeo na wafuasi wake walivamia jengo la bunge au Congress.

Wakati huu, msukosuko unaweza kuwa mbaya zaidi. Trump anapoendelea kudai kuwa hana imani na taasisi za serikali na kusisitiza kuzisafisha, iwapo atashinda.

Lakini ikitokea akipigwa tena, hasira yake inaweza kumfanya sio tu kukataa matokeo, bali atangaze ushindi moja kwa moja, na kuiacha Marekani na marais wateule wawili wakihangaika kupata kutambuliwa ndani na nje ya nchi.

Hali hii inaweza kusababisha mifarakano katika nchi hiyo ambayo wengi wanaiita polisi wa dunia.

Wiki iliyopita tofauti kati ya Kamala na Trump ilikuwa finyu lakini sasa hakuna mbadala . Allan Lichtman, mtabiri wa urais ambaye ametabiri kwa usahihi matokeo ya chaguzi zote za urais tangu 1984, anampa ushindi wa Kamala akisema kwa hesabu yake, Makamu wa Rais huangalia mambo nane muhimu, ambayo yanatosha kushinda.

Kwa upande mwingine, kura nyingi za maoni na utabiri zinatabiri ushindi mwembamba wa Trump.



## Wakulima waitwa kujisajili ili kulinda bidhaa zao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) umewataka wakulima nchini pamoja na wazalishaji wa bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo kusajili nembo za bidhaa zao ili kuzilinda zisichakachuliwe.

Ofisa Usajili BRELA, Gabriel Barangay, alitoa wito huo juzi jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu shughuli mbalimbali wanazozifanya kwenye Maonesho ya Wakulima ya Nanenane yanayoendelea kwenye Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Barangay alisema, wakulima wengi nchini wanalima mazao na kuongeza thamani lakini hawana usajili wa nembo za bidhaa zao zitokanazo na mazao ya kilimo.

"Wakulima ni wadau wetu muhimu sana kwani wengi wanalima mazao kama mahindi na kuongeza thamani kwa kusaga unga na kufungasha kwenye mifuko, lakini wengi wao hawana usajili wa majina ya nembo za bidhaa zao hivyo tunatoa wito kwao kuja kwetu ili kupata usajili wa 'brand' za bidhaa zao" alisema.

Alisema lengo la BRELA ni kuwasaidia wakulima kusajili biashara zao rasmi ili kuwa na usajili wa kampuni, ushirika au biashara ndogondogo zinazohusiana na kilimo.

Alisema pia BRELA hutoa huduma hizo ili kuhakikisha biashara za kilimo zinakubalika kisheria ikiwa na kutoa ushauri kuhusu jinsi ya kufuata taratibu za kisheria pamoja na kanuni za usajili, sheria za biashara na masharti ya leseni.

# Waletewa programu kuongeza uzalishaji kahawa na wenye tija

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kahawa ya Tanzania (TaCRI), inatekeleza programu maalumu ya kuwawezesha wakulima kufuata kanuni za kilimo zinazopendekezwa ili kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa na wenye tija kwa ajili ya kibiashara.

Kupitia programu hiyo madhubuti ambayo imeanza kuleta matokeo yenye tija kwa wakulima wengi wa kahawa. Wataalamu wa kilimo kutoka TaCRI wanawafundisha wakulima mbinu mbalimbali ili kusaidia kuongeza uzalishaji na wenye tija.

Kuanza kutolewa kwa mafunzo hayo kumetokana na utafiti uliofanywa ambapo walibaini kuwa, asilimia kubwa ya wakulima wa zao hilo nchini wanalima kienyeji jambo linalosababisha kutoa mavuno kidogo.

Katika kuboresha ufanisi wa mkulima, Meneja wa Shamba la TaCRI, Melchior Tesha amesema, wameamua kutoa mafunzo maalumu kwa lengo la kuwasaidia wakulima wa kahawa, kulima kwa kuzingatia kilimo cha za kisasa.

"Miongoni mwa kanuni za kisasa za kilimo, tunazowafundisha ni namna bora ya kulima kilimo cha mseto, kinacho jumuisha upandaji wa miti ya vivuli katika mashamba ya kahawa," alisema.

Alitaja miti inayopendekezwa kupandwa kuwa ni aina ya mruka na mringaringa, miti ambayo amesema ni muhimu katika kutoa kivuli kwa mimea ya kahawa, lakini pia katika kusaidia kufunika udongo kwa madhumuni ya kuhifadhi unyevunyevu.

"Miti hii ina faida nyingi kwa sababu mbali na kusaidia ukuaji wa mimea ya kahawa, inawawezesha wakulima kupata chakula cha mifugo, mbao pamoja na kuni," alieleza.

Pamoja na hayo, alisema upandaji wa miti hiyo inawasaidia wakulima kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Mbinu nyingine ambazo taasisi hiyo inawafunza wakulima kwa ajili ya kuwasaidia kuzalisha zao hilo kwa manufaa zaidi ni matumizi ya kilimo mseto cha kahawa na migomba, ambapo wakulima hunufaika maradufu kwa kuzalisha na kuuza mazao yote mawili ya kibiashara, kahawa na ndizi.

"Katika mpango huo, TaCRI pia inatoa mafunzo kwa wakulima kulima mikunde katika mashamba yao ya kahawa," alisema.

Aliongeza kuwa, mazao yanayopendekezwa kulimwa pamoja na kahawa hayashindani katika kutafuta chakula na kahawa wala kuambukizana magonjwa.

Usimamizi wa udongo na uvunaji wa maji ni miongoni mwa njia nyingine ambazo programu inawafunza wakulima ili kulikuza zao hilo kibiashara.

Tesha, aliongeza kuwa programu hiyo, pia ina jukumu kubwa katika kutoa mafunzo kwa wakulima kutumia ipasavyo matumizi ya vidhibiti wadudu vinavyopendekezwa.

Alisema kwa mujibu wa kilimo cha kahawa kitaalamu, mti mmoja wa kahawa unatakiwa kuwa na matawi kati ya 45 na 48, ambapo ekari moja lazima iwe na ujumla ya mimea 1,330.



Meneja Mkuu wa Biashara wa Benki ya Equity Tanzania, Leah Ayoub (kushoto), akibadilishana mkataba na Mkurugenzi wa Shirika la Private Agricultural Sector Support (PASS), Adam Kamanda, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ya kuwasaidia mikopo wakulima nchini, katika Maonesho ya Kilimo Nanenane, Nzuguni jijini Dodoma jana. Katikati ni Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima 100,000 sasa kupata mikopo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAKULIMA zaidi ya 100,000 wanatarajiwa kunufaika na mikopo inayotolewa na Benki ya Equity Tanzania kupitia udhamini wa Shirika la Private Agricultural Sector Support (PASS).

Mkurungenzi wa Biashara wa PASS, Adam Kamanda, alisema hayo baada ya shirika hilo kusaini mkataba wa makubaliano na benki hiyo kwenye viwanja vya maonesho ya Nanenane yanayoendelea Viwanja vya Nzuguni, tukio lililoshuhudiwa na Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde.

Kamanda alisema kupitia mkataba huo, utawasaidia wakulima hapa nchini zaidi ya laki moja kunufaika na mikopo hiyo inayotolewa kwa udhamini wao.

Kadhalika, alisema hadi sasa kuna watu zaidi ya 30,000 wameanza kunufaika na mikopo hiyo inayotolewa na taasisi hiyo ya kifedha kwa udhamini wa PASS.

Alibainisha kuwa, shirika hilo linafanyakazi katika mikoa yote nchini, hivyo wakulima wanaohitaji mikopo watanufaika kwa kupata ufadhili huo.

Alisema mikopo hiyo itawasaidia wakulima hao kutumia mikopo hiyo kununua mbegu bora ili kusaidia kuboresha maisha ya kundi hilo ambalo wamekuwa wakipata tatizo la kupata mikopo kwa masharti nafuu.

Pia alisema PASS imekuwa ikitoa udhamini kwa kundi la wajasiriamali wadogo na wakubwa ili kuboresha maisha ya kundi hilo.

Meneja Mkuu wa Biashara wa Equity Tanzania, Leah Ayoub, alisema mkataba huo unalenga kusaidia sekta ya kilimo ambayo inatoa ajira kwa watu wengi.

Leah alisema, mikopo hiyo itakuwa na masharti nafuu na itakuwa na riba ndogo na italenga wakulima wa maeneo ya vijijini ambao wamekuwa na tatizo la kukosa dhamana ya mikopo.

Aliongeza kuwa, wanakusudia kuwafikia wakulima wengi zaidi kutokana na udhamini huo ambao wamesaini na PASS.

Mkurungenzi wa Shirika la Movement for Community Development (Mcode), Slaiton Kaberege, ambapo shirika lake pia lilisaini mkataba na benki hiyo, alisema mkopo huo utawasaidia wakulima wa Kanda za Juu Kusini kuinuka kiuchumi.

Aidha, Berege alisema fedha hizo zitawasaidia wakulima wa mikoa sita ambayo ni Iringa, Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa.

Alisema shirika hilo limekuwa likishirikiana na benki hiyo na kutoa mikopo. Aliongeza kwa kusema kuwa, kuna vikundi zaidi ya 1,000 vimeanza kunufaika na mikopo hiyo.



# Matumizi ya mbolea bado tatizo kwa wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA kutoka mikoa 14 nchini wanadaiwa kuwa na mwamko mdogo wa matumizi ya mbolea, hali ambayo inasababisha tija ya uzalishaji wa mazao kuwa chini ikilinganishwa na ukubwa wa mashamba yanayolimwa.

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'ondya alisema hayo jijini Mbeya kwenye Maonesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini alipokuwa anatoa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Lindi, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Mara, Mwanza, Simiyu, Geita, Kagera, Shinyanga, Ruvuma na Katavi na kwamba tatizo kubwa lipo kwenye mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alisema kutokana na tatizo hilo, mamlaka hiyo imezindua kampeni maalumu iitwayo' kilimo ni mbolea' ambayo inalenga kuhamasisha wananchi wa maeneo hayo kutumia mbolea kwa usahihi.

Alisema kampeni hiyo ilizinduliwa Mei mwaka huu katika Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma ambako ni miongoni mwa mikoa michache ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ina tatizo hilo.

"Matumizi haya hafifu ya mbolea kwenye mikoa hii yanasababisha wakulima wa maeneo hayo kulima maeneo makubwa huku uzalishaji kuwa mdogo, sasa kampeni hii inakwenda kubadili mtazamo na kuongeza matumizi," alisema Ng'ondya.

Alisema waliamua kuanzisha kampeni hiyo kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya ardhi hali ambayo inasababisha maeneo ya kilimo kupungua na hivyo kuhitaji mabadiliko ya teknolojia.

Alisema watu wakianza kutumia mbolea kwa usahihi watakuwa wanalima maeneo madogo na uzalishaji kuwa mkubwa na kuwa na utoshelevu wa chakula na ziada kuuza.

Hata hivyo baadhi ya wananchi waliishukuru serikali kwa kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo hasa mbolea wakidai kuwa imewasaidia kupunguza bei ya bidhaa hiyo.

Mmoja wa wakulima hao, Sebastian Mbunda, alisema kabla ya serikali kuweka ruzuku kwenye mbolea imewasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kuongeza matumizi ya mbolea.

Alisema katika Mkoa wa Ruvuma ambako yeye ana mashamba msimu uliopita walikuwa wananunua mbolea za kupandia kwa Sh. 70,000 badala ya 120,000 ambayo ilikuwapo kwenye msimu wa mwaka juzi.

"Tulikuwa tunapata shida kubwa sana ya kupata mbolea, wengi sana tulishindwa kutumia mbolea kwa hiyo tuliishia kulima mazao yetu mengi lakini tukashindwa kuhudumia kwa sababu bei ya mbolea ilikuwa juu sana," alisema Mbunda.

Alipokuwa anafunga maonyesho hayo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko aliagiza Wizara ya Kilimo na wadau mbalimbali kuongeza juhudi ya kutoa elimu ya matumizi ya mbolea kwa wakulima ili kuongeza tija ya uzalishaji.



Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni, Elizabeth Mokiwa, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Aprili hadi Juni, mwaka huu, ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 8. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Serikali yatakiwa kutanua wigo mikopo vyuo vya kati

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

SERIKALI imeshauriwa kutanua wigo wa mikopo ya elimu ya vyuo vya kati badala ya kujikita kwenye kozi chache za kipaumbele, ili kunusuru ndoto za watoto wanaotoka kwenye familia maskini ambao wanashindwa kusoma kutokana na kukosa ada.

Ushauri huo umetolewa na Mkuu wa Chuo cha Afya Lugarawa (LUHETI) kilichopo katika Wilaya ya Ludemwa mkoani Njombe, Buteye Dotto wakati wa mahafali ya 24 ya chuo hicho.

Alisema kuna baadhi ya wanafunzi wakiwamo wa kike ambao wamekuwa wakijiingiza kwenye biashara ya ngono na wengine kushindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya kutomudu mahitaji ya chuoni.

Aidha, aliiomba serikali kutanua wigo wa kozi zinazonufaika na mikopo ili kuokoa ndoto zinazokufa kwa kushindwa kuendelea na masomo.

"Tunaishukuru serikali kwa kuona kwamba vijana hawa wanahitaji sapoti, tunaomba iweze pia kuangalia kwa hizi kozi nyingine," alisema Dotto.

Awali Askofu wa Jimbo Katoliki la Njombe, Eusebio Kyando, aliwakumbusha wahitimu hao kufanya kazi ya kuhudumia watu kwa kuzingatia kiapo na maadili.

Mkurugenzi wa Chuo cha Afya Lugarawa, Padri Alexanda Mlelwa, aliiomba serikali kutazama kwa jicho la tatu tatizo la ajira nchini hasa katika kada ya afya.

"Nilimsikiliza Waziri wa Afya wiki iliyopita akasema kuna ukosefu wa wahudumu wa afya asilimia 50 na sababu alizosema ni nzuri tu kwamba serikali imejenga vituo vingi vya afya na hivyo inakosa wahudumu," alisema Mlelwa.

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda alisema serikali itaendelea kuajiri watumishi katika kada ya afya kwa kuwa imejenga vituo vya afya vingi na hospitali ambapo amewataka wahitimu kuanza kwa kujitolea kipindi wanachosubiri ajira.

Mmoja wa wahitimu hao akiwamo, Brenda Shayo alisema kuna tatizo kwenye upande wa vyuo vya kati hasa upande wa ada hivyo kusababisha kujihusisha na vitendo vya ngono na kushindwa kutimiza ndoto zao za kupata elimu.

## RC Mtaka akoshwa uongezaji thamani mazao

**Na Elizabeth John,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amesema kumekuwa na mwitikio mkubwa na uelewa mpana wa watu kupunguza kuuza vitu ghafi badala yake wanaongeza thamani kwenye mazao.

Mtaka aliyasema hayo juzi wakati akikagua mabanda katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane) kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika viwanja vya John Mwakangale jijini hapo.

Alisema hali hiyo imetokana na uwepo wa uonyeshaji wa teknolojia za kisasa zinazoweza kumsaidia mkulima anayefanya shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya kilimo kwa sababu ya uwepo wa taasisi za kifedha ambazo zitatoa kipaumbele kwa wakulima kwa kuwapatia mikopo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sanday Deogratias, alisema bado wajasiriamali wanakabiliwa na tatizo la kupata mitaji ili waweze kuongeza thamani vitu wanavyozalisha.

Alisema: "Rai yangu ni kwamba taasisi zote za fedha zina mikopo mbalimbali kwa hiyo wajitahidi kutoa elimu ili kuwafikia wakulima wote na wafugaji ili kuweza kupata mikopo hiyo," alisema Deogratias.

Meneja wa mkakati wa bidhaa na masoko kutoka Kampuni ya One Acre Fund, Eric Ballegu alisema hivi sasa kuna mwitikio mkubwa wa wakulima kupima udogo ambapo huko nyuma walishindwa kutokana na gharama kuwa kubwa.



## Waitwa Tamasha la Kizimkazi kujifunza mila, utamaduni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kushiriki katika Tamasha la Kizimkazi Festival ili kujifunza mila, utamaduni na silka za kitanzania.

Mwenyekiti wa tamasha hilo, Mahfoudh Said Omar, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari Kizimkazi Mkunguni Mkoa wa Kusini Unguja kuhusu maandalizi ya tamasha hilo ambalo linatafunguliwa mwezi huu.

Alisema tamasha hilo la aina yake litajumuisha shughuli nyingi ikiwamo uwekaji wa jiwe la msingi katika Chuo cha Michezo cha Samia Suluhu Hassan ambacho kinategemewa kuwa chemchemu ya kuibua vipaji.

Aidha, alisema tamasha hilo ambalo litaanza Agosti 18, hadi Agosti 25 mwaka huu litakuwa na shughuli mbalimbali za kimaendeleo, kiuchumi na burudani, ambao utaambana na ufunguzi wa miradi, michezo, vyakula vya asili na mashindano ya kuibua vipaji.

Alisema lengo la tamasha hilo ni kuutangazia umma shughuli mbalimbali za kimila, kijadi na kiutamaduni ili wananchi wa mataifa mbalimbali kufahamu mila za Tanzania.

Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii Tanzania, Ephrahim Mafuru, alisema kupitia tamasha hilo litashirikisha wadau upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ambalo litachangia pato la taifa na kipato cha mtu.

Alisema kuwa vijana watapata fursa ya kupata elimu ya kuwawezesha kupata kipato chao kwa ajili ya maendeleo.

Naye Katibu wa tamasha hilo, Hamid Abdulhamid Khamis, alisema watatoa mafunzo kwa vijana 500 ambapo watakuwa katika makundi matano ikiwamo ujasiriamali, uvuvi, kilimo, sanaa na utalii.

Mwanzilishi wa tamasha hilo, Said Hamad Ramadhan, alisema walianzisha miaka nane iliyopita kwa lengo la kuimarisha utamaduni na historia ya Mkoa wa Kusini.

Alisema tathmini ya tamasha hilo linaonesha kukua kwa kasi kutokana na maandalizi makubwa yaliofanyika na shughuli zilizoandaliwa.

Tamasha hilo litafunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.Hussein Ali Mwinyi na kilele chake kitafungwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

# Mazrui avunja ukimya kutoonekana jukwaani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Nassor Ahmed Mazrui, amesema yeye kutoonekana katika majukwaa ya mikutano ya hadhara ya chama hicho hakuna maana ya kwamba amehama chama.

Akizungumza na Nipashe visiwani Zanzibar, Mazrui alisema bado yupo katika chama hicho na wala hana mpango wa kuhama.

Mazrui ambaye ni Waziri wa Afya, alisema kuwa licha ya kutoonekana katika baadhi ya mikutano ya hadhara ya chama hicho inayoendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba lakini bado anamchango mkubwa katika chama.

"Mimi bado ni mwanachama wa ACT-Wazalendo na wala sina mpango wa kuhama, nimetingwa tu na majukumu mingine, ndiyo maana wanachama hawajaniona katika mikutano lakini wataniona katika majukwaa," alisema Mazrui.

Aidha, alisema licha ya kwamba kwa sasa hana nafasi yoyote ya uongozi katika chama baada ya kutogombea tena katika uchaguzi uliopita wa chama hicho, lakini bado anaendelea kushirikiana na viongozi wa chama katika kukiimarisha chama hicho.

Wakati hayo yakiendelea, hivi karibu katika ufunguzi na makabidhiano ya nyumba za wafanyakazi Hospitali ya Abdulla Mzee Mkoa wa Kusini Pemba, Waziri Mazrui alionekana kuwafurahisha viongozi na wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi kwa kusifu kazi kubwa inayofanywa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi kwa kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi CCM ya mwaka 2020/2025 katika sekta ya afya nchini.

Kauli hiyo ya Waziri Mazrui pia ilionekana kuwakwaza baadhi ya wafuasi na viongozi wa chama chake, ambapo alikiri kupokea malalamiko kutoka kwa wafuasi wa chama hicho kwa kumsifia Dk. Mwinyi hadharani.

Lakini alipokea pongezi kutoka kwa wafuasi wa CCM na kupokea maombi ya kwamba ajiunge CCM.



Mafundi wakiziba bomba la majisafi lililopasuka wakati wa ujenzi unaoendelea wa barabara ya Mnazi Mmoja hadi Kikwajuni Baraza la Wawakikishi la zamani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Dk. Mwinyi aagiza uboreshaji maabara, wataalamu ZBS

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameiagiza Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), kuhakikisha kuwa na maabara za kisasa na wataalamu wenye uwezo katika kazi za upimaji na ukaguzi wa bidhaa zote nchini.

Alisema hayo jana baada ya kufungua kituo kipya cha ukaguzi wa vyombo vya moto eneo la Maruhubi kwenye ofisi za ZBS Mjini Unguja.

Alisema hatua hiyo itawezesha kulinda afya na usalama wa nchi, kuhifadhi mazingira, kuweka ushindani sawa na mazingira wezeshi ya kufanya biashara na kuviwezesha viwanda vya ndani kuzalisha bidhaa zenye viwango.

Dk. Mwinyi alisema kwa lengo la kufikia hatua hiyo serikali inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha miundombinu ya ubora ya ZBS, kwamba miongoni mwa hatua hizo ni kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto.

Aidha, alisema suala la viwango na udhibiti wa ubora siyo geni tena Zanzibar na serikali inaendelea kusimamia suala hilo kwa lengo la kuhakikisha Zanzibar haigeuzwi kuwa sehemu ya bidhaa zisizokidhi viwango ikiwamo vyombo vya moto.

Dk. Mwinyi alisema ni dhahiri kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha vyombo vya moto vinakaguliwa na kuthibitishwa ubora wake kwa ajili ya matumizi ya barabarani.

Alisema vyombo hivyo vinapokosa ubora hupelekea kutokea kwa madhara mbalimbali yakiwamo ya uchafuzi wa hali ya hewa unaotokana na moshi na ajali za mara kwa mara ambazo huchangia kupoteza nguvu kazi ya taifa na serikali hutumia fedha nyingi katika sekta ya afya kwa kutoa matibabu kwa wahanga wa ajali hizo.

Alisema kituo hicho kitaongeza uwezo na ufanisi katika ukaguzi wa vyombo vya moto ambapo itapelekea kuwa na vyombo vya moto salama na vinavyofaa kwa matumizi.

Hivyo, aliwataka watendaji wa ZBS kuvitunza vifaa vilivyomo katika kituo hicho ili kuendelea kufanya kazi na wafanyakazi kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya kuwapa huduma bora wananchi.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema takwimu zinaonesha kuwa uingiaji wa vyombo vya moto umeongezeka kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na miaka iliyopita.

Alizitaka mamlaka zinahusika na upasishaji wa vyombo vya moto kuendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo ili malengo makuu ya usalama, ubora na viwango vya vyombo vya moto vinavyofika nchini viweze kufikiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yusuph Majid Nassor, alisema lengo la kujengwa kwa kituo hicho ni kuondoa kadhia za wananchi kwenda kwenye taasisi za umma kwa ajili ya kufanya usajili wa vyombo vyao vya moto katika sehemu mbalimbali.

Alisema ndani ya kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto imefungwa mitambo miwili yenye uwezo wa kukagua magari 300 kwa siku.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ABEL THOMAS LYIMO** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE244059** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji DAR ES SALAAM. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/163786/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GUTA

**MARKI OMARY NURDIN** ANATANGAZWA KUPOTELEWA NA KADI YA **GUTA** YENYE NAMBA YA USAJILI **MC 511 CHE** ILIYOPOTEA HIVYO KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/11677/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRAIG WELLOUGHBY WOOD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 899 AZD – SUZUKI GRAND VITARA** yenye Chassis namba **JSAJTDA4V00110828.** Engine namba **J24B1021044.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/162710/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HUBERT NESTOR ILAHUKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 768 CBU – TOYOTA SPRINTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/158909/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MAUA PYRETHRUM LTD** WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI **MC254 CQG** AINA YA KINGLION , KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/KIL/11733/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RASHID RASHID LIKOMBOLEKA** natangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 294 CCJ TVS STAR, CHASISS NO.MD625AF40J1877** na ENGINE **NO.DF4LJ1XA5215.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/MTW/MTW/4420/2024**

## KUPOTEA KWA LESENI YA MAKAZI

**DEONIS PROSPER MUTAGWABA** anatangaza kupotea kwa leseni ya makazi yenye namba **TMK015715** na KIWANJA NAMBA: **TMK/MBGL/KNY22/420.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/130896/2024**

E.R.PALLANGYO
MSAJILI MSAIDIZI WA NYARAKA
MANISPAA YA TEMEKE

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 18519 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**JOHNPAUL AMON BYEJWE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**ADAM AMON BYEJWE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 30TH day of August 2024

Dated at Dodoma this 6th day of August, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**FORM 58**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

**IN THE COURT DISTRICT DELEGATE OF ARUSHA DISTRICT**
**AT ARUSHA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 1730 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late AGNES DENIS KAFURIA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR PROBATE OF THE WILL OF THE LATE**

**BY ERICK DENNIS KAFURIA**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate is made to the above –named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 9 th Day of AUGUST, 2024

The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court.

Date at ARUSHA this 24TH Day of JULY, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Iran yatishia kuishambulia Israel

**TEHRAN,** Iran

IRAN imesema kuwa, ina haki kisheria ya kuiadhibu Israel kutokana na mauaji ya wiki iliyopita ya kiongozi wa kisiasa wa kundi la Hamas, Ismail Haniyeh yaliyotokea katika mji mkuu wa taifa hilo Tehran.

Serikali ya Iran jana iliapa kuwa italipiza kisasi baada ya mauaji ya kiongozi huyo, licha ya Israel kutozungumzia tukio hilo, wakati ikishutumiwa na Tehran kuhusika na mauaji hayo.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Iran, Nasser Kanani, alisema nchi hiyo haina nia ya kulitumbukiza eneo la Mashariki ya Kati kwenye vita kamili, lakini wanapozungumzia kuhusu haki yao ya kuiadhibu Israel, hiyo ni hatua ya kusaidia kuimarisha usalama na utulivu katika eneo hilo.

**Tunaamini kuwa, uimarishwaji wa usalama uliothabiti katika eneo hili, utafikiwa kwa kumwadhibu mvamizi huyo na kuweka kizuizi dhidi ya tabia yake ya uhasama na vitisho vya utawala wa kizayuni hadi nje ya mipaka yake.**

"Tunaamini kuwa, uimarishwaji wa usalama uliothabiti katika eneo hili, utafikiwa kwa kumwadhibu mvamizi huyo na kuweka kizuizi dhidi ya tabia yake ya uhasama na vitisho vya utawala wa kizayuni hadi nje ya mipaka yake," alisema.

Ilielezwa kuwa, hofu imekuwa ikiongezeka katika eneo zima la Mashariki ya Kati ambapo linaweza kutumbukia kwenye vita kamili, wakati mataifa kadhaa yakiwataka raia wake kuondoka na kutosafiri kuelekea Lebanon, huku wanadiplomasia wa kimataifa wakiendeleza juhudi za kupunguza hali ya mvutano.

Katibu wa Baraza la Usalama la Taifa la Russia, Sergei Shoigu ambaye alikuwa waziri wa zamani wa ulinzi wa taifa hilo, aliwasili jana Tehran, wakati kukiwa na hofu ya vita vikubwa katika eneo hilo.

Ilielezwa kuwa, anatarajiwa kukutana na maofisa wakuu wa kijeshi na kiusalama pamoja na kufanya mazungumzo na Rais mpya, Masoud Pezeshkian ili kujadili namna ya kuimarisha ushirikiano katika nyanja mbalimbali ikiwamo suala la usalama.

Russia ambayo ni mshirika wa Iran ililaani vikali mauaji ya Hanniyeh na sasa ziara hii ya Shoigu inaweza kutafsiriwa kama ishara ya uungwaji mkono kwa Iran wakati ambako Marekani imesema mara kadhaa kuwa iko tayari kuilinda Israel na vitisho vyote kutoka Iran, huku Rais Pezeshkian wa Iran akisema Russia ni mshirika wa kimkakati anayethaminiwa.

Katika hatua nyingine, Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayehusika na masuala ya Haki za Kibinadamu, Volker Turk, alitoa wito jana akitaka kusitishwa haraka kwa hali ya mvutano huko Mashariki ya Kati kutokana na hofu kwamba vita vya Gaza vinaweza kutanuka zaidi.

Turk ameyataka mataifa yenye ushawishi kuchukua hatua za haraka ili kukomesha hali ambayo ameitaja kuwa hatari na kusema katika kipindi cha miezi 10 iliyopita, raia wengi wakiwamo wanawake na watoto, wamepitia madhila na mateso yasiyovumilika kutokana na vita vinavyoendelea huko Mashariki ya Kati. **DW**

## Waziri Mkuu Bangladesh akimbia nchi

**DHAKA,** Bangladesh

WAZIRI Mkuu wa Bangladesh, Sheikh Hasina, amejiuzulu na kukimbia taifa hilo kutokana na machafuko yanayosababishwa na maandamano ya vijana yanayoendelea nchini humo yakipinga utaratibu wa serikali katika utoaji ajira.

Hayo yalibainishwa jana nchini humo na Mkuu wa Jeshi la Bangladesh, Jenerali Waker-Uz-Zaman, na kwamba taifa hilo litaongozwa na Jeshi kwa muda, huku ikidaiwa kuwa waziri huyo amekimbilia India wakati akijiandaa kuhamia taifa lingine.

Bangladesh imekumbwa na maandamano na ghasia zilizoanza mwezi uliopita baada ya makundi ya wanafunzi kutaka kufutwa kwa mfumo tata wa kupeana nafasi za kazi serikalini kwa jamaa za watu waliopigania uhuru wa nchi hiyo, na hadi sasa watu 250 wameuawa.

Ilielezwa kuwa hilo liliongezeka na kuwa kampeni ya kutaka kuondolewa madarakani kwa Hasina, ambaye amekuwa madarakani kwa miaka 15 na ikumbukwe Januari mwaka huu alishinda muhula wa nne mfululizo.

Katika hatua nyingine ilielezwa kuwa, kabla ya kuwa Mkuu wa Jeshi, alihudumu kama Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi kwa zaidi ya miezi sita jukumu ambalo alisimamia operesheni za kijeshi na ujasusi, jukumu la Bangladesh katika operesheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa (UN) na bajeti.

Katika huduma yake jeshini iliyodumu miongo mitatu na nusu, pia amefanya kazi kwa karibu na Hasina, akihudumu kama Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Jeshi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. **BBC**



Waandamanaji wakiwa wameizingira nyumba ya Waziri Mkuu wa Bangladesh, Sheikh Hasina, baada ya kujiuzulu na kukimbilia uhamishoni, jana. **PICHA: MTANDAO**

## Polisi wa DRC wakimbilia Uganda

**KINSHASA,** DRC

MAOFISA 100 wa polisi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wamekimbilia nchini Uganda wakati mapigano kati ya waasi wa M23 na wanajeshi, Mashariki mwa taifa hilo yakizidi kuongezeka.

Hayo yalibainishwa jana na Msemaji wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Uganda, Meja Kiconco Tabaro, ikieleza kuwa maofisa hao waliwasili kupitia kivuko cha mpaka cha Ishasha katika Wilaya ya Kanungu Kusini Magharibi mwa Uganda. Alisema maofisa hao walifika wakiwa na bunduki 43 zenye risasi ambazo baadaye walipokonywa.

"Walikuwa wakikimbia mapigano na M23 na wanamgambo wengine na Jeshi la Kongo, kuna vurugu nyingi huko na kuna njaa. Na katika muda wa siku nne zilizopita takriban wakimbizi 2,500 zaidi wa nchini humo wamewasili Uganda wakikimbia ghasia zinazoendelea kuvuka mpaka," alisema Meja Tabaro.

Kundi la M23 limekuwa likiendesha uasi wake katika eneo la Mashariki, linaloundwa na wanamgambo wa Kongo tangu 2022. Ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN) iliyoonekana na Reuters mwezi uliopita ilisema Jeshi la Uganda limetoa msaada kwa kundi la waasi linaloongozwa na Watutsi, madai ambayo Uganda inakanusha.

UN imeishutumu kwa muda mrefu Rwanda kwa kuunga mkono kundi la M23, ambalo mara kadhaa limeteka sehemu kubwa ya eneo lenye utajiri wa madini Mashariki mwa Kongo, madai ambayo Rwanda ilikanusha pia.

Juhudi za Jeshi la Kongo kuwarudisha nyuma waasi hao zimeongezeka katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita kwa kutumia ndege zisizo na rubani ingawa waasi hao bado wamepanua maeneo chini ya udhibiti wao.

Mwezi Juni, M23 waliuteka mji wa Kanyabayonga, ambao eneo lake kwenye eneo la juu linaifanya kuwa lango linalotumiwa kuelekea maeneo mengine ya Mashariki mwa Congo ya Jimbo la Kivu Kaskazini. Mapigano huko Kivu Kaskazini yamewafukuza zaidi ya watu milioni 1.7 kutoka makwao, na kusababisha jumla ya Wakongo waliokimbia makazi kutokana na migogoro mingi kufikia milioni 7.2 kulingana na makadirio ya UN. **TRT AFRIKA**

HABARI MICHEZO

# AZAM YATUA ZENJI KIBABE KUIKABILI COASTAL UNION

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Azam FC, kiliwasili jana jioni mjini Zanzibar tayari kwa mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Coastal Union, utakaopigwa saa 10:00 jioni, Uwanja wa New Amaan Complex mjini humo.

Kikosi hicho kiliondoka Dar es Salaam jana saa 10:00 jioni kwenda Zanzibar, ikiwa ni siku moja tu baada ya kurejea kutoka nchini Rwanda ilikokwenda kucheza mchezo wa kirafiki wa kimataifa na kushinda bao 1-0 dhidi ya Rayon Sport.

Kabla ya kwenda huko, Azam ilikuwa nchini Morocco kwa ajili ya maandalizi ya msimu, 'pre season' kwa kiasi cha wiki tatu.

**Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hasheem Ibwe, amesema kikosi chao kipo imara kwa ajili ya mchezo huo licha ya kwamba utakuwa mgumu kutokana na historia ya rekodi za timu hizo mbili zinapokutana.**

"Itakuwa mechi nzuri, mechi dume ni mechi ambayo itaamua timu itakayokwenda kucheza fainali au kusaka mshindi wa tatu, kwa namna ambavyo tumejiandaa pamoja na timu yetu ilivyo tuna matumaini ya kufanya vizuri, tuna timu nzuri, kikosi kimekamilika tunategemea kuwa na mchezo mzuri," alisema Ofisa Habari huyo.

Hata hivyo alikiri kuwa hautokuwa mchezo rahisi kutokana na kuwa hupata wakati mgumu sana wanapocheza na Coastal Union.

"Coastal ni timu ngumu, na huwa wanatupa wakati mgumu sana tunapocheza nao, tumewafunga mara moja tu kwenye Ligi Kuu tena msimu uliopita bao 1-0, Uwanja wa Mkwakwani Tanga na ulikuwa mchezo mgumu sana, kwa hiyo si rahisi kucheza nayo hata kidogo," alisema.

Coastal ipo Zanzibar kwa muda sasa ambako imeweka kambi yake ya 'pre season' kujiandaa na Ligi Kuu, Ngao ya Jamii, pamoja na Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Juzi kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, timu hiyo ilicheza dhidi ya Uhamiaji ambayo itacheza dhidi ya Simba kama itaifunga Al Ahly Tripoli ya Libya kwenye mechi za Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Coastal ilishinda mabao 2-0, yaliyowekwa wavuni na Abdallah Hassan na Denis Modzaka.



Mchezaji wa Timu ya Videte Center, Alfan Hamis (kulia), akiwania mpira na mchezaji wa Timu ya Maginja FC, Haji Abeid, walipokuwa wakicheza mechi ya kirafika katika Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mbio za mbuzi kukusanya mil. 400/- kusaidia elimu

**Na Mary Geofrey**

KLABU ya Rotary Oysterbay Dar es Salaam, inatarajia kukusanya zaidi ya milioni 400 kwa ajili ya kusomesha wanafunzi wa elimu ya juu, kupitia tamasha la mbio za mbuzi litakalofanyika Septemba 7, mwaka huu.

Rais wa klabu ya Rotary Oysterbay, Himanshu Bhattbhatt, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tamasha hilo, lililodhaminiwa na Kampuni ya Simu ya Vodacom.

Alisema tamasha hilo linalotarajia kuhusisha washiriki 4,000, litafanyika kwa mara ya saba tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018, kwa lengo la kushirikiana na serikali kuboresha sekta ya elimu nchini.

"Mbio za mbuzi mwaka huu zitafanyika Septemba 7 katika Viwanja vya The Green Oysterbay jijini Dar es Salaam kuanzia saa 6:00 mchana hadi saa 2:00 usiku," alisema Bhattbhatt.

Alisema kupitia tamasha hilo, washiriki ambao ni watu wazima na watoto watapata burudani mbalimbali kupitia michezo iliyoandaliwa.

Naye Mkuu wa Uhusiano kwa Umma na Vyombo vya Habari wa Vodacom, Annette Kanora, alisema kampuni hiyo imejikita kwenye kutumia ubunifu wa aina mbalimbali ili kuisaidia jamii katika kuiletea maendeleo.

"Baada ya kuona mafanikio yaliyotokana na mbio za mbuzi za mwaka 2023, kampuni imevutiwa kuendelea kudhamini mbio hizi za hisani kwa mwaka wa pili mfululizo," alisema Annette.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa sekta ya elimu nchini, Vodacom na klabu ya Rotary Oysterbay wanaweza kuboresha mazingira ya elimu, kutoa ufadhili wa elimu kwa wanafunzi wenye uhitaji na kuimarisha miundombinu ya maji na usafi shuleni.

## Waendesha baiskeli Afrika Mashariki watua Ngara

**Na Judith Julius,** Ngara

MSAFARA wa waendesha baiskeli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wakitokea nchini Burundi wanaoshiriki katika mbio za 'Great Africa Cycling Safari', umewasili Tanzania.

Waendesha baiskeli hao walipokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Julius na mapokezi hayo yalifanyika katika mpaka wa Tanzania na Burundi eneo la Kabanga.

Waendesha baiskeli hao kutoka nchi wanachama wa EAC watazunguka nchi za Jumuiya hiyo zikiwamo, DR Congo, Burundi, Tanzania, Kenya, Uganda na Rwanda.

## *Uwanja kucheza Ligi kuanzia watazamaji 3,000*

**Na Shufaa Lyimo**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) imesema hakuna uwanja utakaoruhusiwa kutumika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Agosti 16, mwaka huu kama hautakuwa na uwezo wa kuingiza watazamaji 3,000.

Hayo yalisemwa jana na Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo wakati alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari katika semina iliyofanyika kwenye kumbi za Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Hatutakubali kuona uwanja ambao hauna majukwaa yenye uwezo wa kuingiza watazamaji elfu tatu (3,000) kutumika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara wala hatutakuwa na huruma na hilo," alisema Kasongo.

Aidha, alisema hiyo ni miongoni mwa kanuni mpya zilizopitishwa hivi karibuni na Bodi hiyo yenye lengo la kuhakikisha Ligi Kuu inazidi kuwa yenye ubora zaidi.

Vile vile alisema kanuni nyingine ni ile ambayo inazitaka timu zinazocheza Ligi Kuu kuhakikisha zinakuwa na wachezaji wawili waliowatoa kwenye timu zao za vijana.

Aidha, alisema anasikitishwa na kitendo kinachofanywa na baadhi ya wasemaji wa timu mbalimbali ambao wamekuwa wakifanya kazi zao bila kufuata maadili ya habari.

Katika hatua nyingine alisema muda wowote wanatarajia kutangaza ratiba mpya ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024-25 ili kila mmoja apate picha halisi ya msimu huo jinsi utakavyokuwa.

"Ratiba ya msimu ujao mpaka sasa imekamilika kwa asilimia 99 ni ratiba ambayo imefanyiwa maboresho makubwa kuhakikisha msimu ujao unakuwa bora zaidi," alisema Mtendaji huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GUEHI AKARIBIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inakaribia kufikia makubaliano ya zaidi ya pauni milioni 60 kumsajili beki wa kati wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24, kutoka Crystal Palace. ***(Telegraph)***

### AGARTE BASI TENA

MANCHESTER United imebadilisha maamuzi kwa kiungo wa kati waliyekuwa wanamtaka kutoka kwa Paris St-Germain raia wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 23. ***(Athleticd)***

### FELIX KWA MKOPO CITY

KLABU ya Atletico Madrid imeipatia Man City mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo kama sehemu ya mkataba wa kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Julian Alvarez mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

### WAN-BISSAKA KUBAKI

MATUMAINI ya West Ham ya kumsajili beki, Aaron Wan-Bissaka yamepata pigo huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akidaiwa kushinikiza malipo ya mamilioni ya pauni kutoka kwa Manchester United ili kuondoka katika klabu hiyo msimu huu. ***(Sun)***

### BREMER AONGEZA MKATABA

KLABU ya Liverpool imepata pigo katika harakati zao za kumnasa mlinzi wa Juventus, Gleison Bremer baada ya Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 27 kusaini mkataba mpya na wababe hao wa Italia. ***(Fabrizio Romano)***

### CHIESA HUYO LIVERPOOL

MATUMAINI ya Liverpool kumpata mshambuliaji, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26 yameimarishwa huku kocha wa Juventus, Thiago Motta akifichua kuwa Muitaliano huyo hana mahitaji kwake. ***(Mirror)***

### OMORODION ASAKWA

CHELSEA ipo kwenye mazungumzo na Atletico Madrid kuhusu mkataba wa karibu pauni milioni 35 kwa mshambuliaji wa Hispania, Samu Omorodion mwenye umri wa miaka 20. ***(Sky Sports)***

### MEC KUTUA CHELSEA

CHELSEA imekubali mkataba wa pauni milioni 20.5 na Gremio kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Gabriel Mec mwenye umri wa miaka 16. ***(Globo)***

### GILCHRIST KWA MKOPO

CHELSEA pia imekubali mkataba wa mkopo wa msimu mzima kwa beki wa Uingereza, Alfie Gilchrist mwenye umri wa miaka 20 kujiunga na Sheffield United. ***(Athletic)***

### ATAKIWA FULHAM

KLABU ya Fulham bado inawasiliana na Manchester United kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27. ***(Sky Sports)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ATLETICO MADRID WAKUBALI KUMNUNUA ALVAREZ WA CITY

**MADRID,** Hispania

**Ataweka rekodi ya kuuzwa kwa bei kubwa zaidi na Manchester City...**

ATLETICO Madrid wamefikia makubaliano na Manchester City kuhusu uhamisho wa Julian Alvarez, kwa mujibu wa 90min.

**Muargentina huyo yuko mbioni kuweka rekodi ya kuuzwa kwa Man City, kwa ada ya pauni milioni 81.5 ikijumuisha nyongeza walizokubaliana na Atletico.**

Gazeti la The Athletic, ambalo lilitangaza kwa mara ya kwanza kuhusu mazungumzo ya juu kati ya Atletico na Man City Jumatatu, liliripoti kuwa klabu hizo mbili zimekamilisha makubaliano.

Alvarez sasa atajadili masuala ya kibinafsi kuhusu kuhamia pale kwenye dimba la Metropolitano na matarajio ni kwamba atatoa mwanga wa kijani kwa uhamisho huo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amekuwa akitangaza kutaka muda zaidi wa kucheza katika wiki za hivi karibuni, licha ya kucheza mechi 103 katika misimu yake miwili akiwa City na kufunga mabao 36.

City ilimsajili Alvarez kutoka River Plate mnamo 2022 kwa pauni milioni 14 na wanaweza kurudisha karibu mara sita ya kiasi hicho ikiwa nyongeza zote zitatimizwa.

Iliripotiwa sana mapema wiki hii kwamba Atletico walikuwa wamebadili mawazo yao kuhusu kumuuza mshambuliaji chipukizi Samu Omorodion kwenda Chelsea kwa takriban pauni milioni 34.4, hivyo kuwapa uhuru wa kumfuatilia Alvarez kwa ukali zaidi.

Atletico ilikataa dau la pauni milioni 27.4 kutoka kwa The Blues hao kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 Juni, lakini dili hilo limerejea na linaweza kukamilika hivi karibuni.

Wakati huo huo, Atletico wanakaribia kuinasa saini ya kiungo wa Chelsea, Conor Gallagher, ambaye anatarajiwa kusafiri kwenda Hispania kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu muda mfupi baada ya kutoa kibali chake cha kuhama.

Gallagher amebakiza mwaka mmoja kukamilisha dili lake la Blues na atajiunga na timu hiyo ya Hispania kwa pauni milioni 34.2.

Atletico tayari wametoa pauni milioni 29.6 kumnunua beki wa kati wa Real Sociedad Robin Le Normand na pauni milioni 27.5 za kumnunua mshambuliaji wa Villarreal Alexander Sorloth.

# KIMMICH: BADO SIJAJUA MUSTAKABALI WANGU



**MUNICH,** Ujerumani

JOSHUA Kimmich amekiri kwamba, kuondoka Bayern Munich bado kunaweza kuwa kwenye karata msimu huu wa joto huku kukiwa na ongezeko la uvumi wa uhamisho wake.

Kiungo huyo mahiri, ambaye alijiunga na Bayern mwaka 2015, alicheza mechi 43 kwa wababe hao wa Bundesliga msimu uliopita, akisajili mabao mawili na asisti 10 hasa akicheza nafasi ya beki wa kulia.

Ilikuwa kampeni ya chini kwa chini kwa Bavaria kumaliza katika nafasi ya tatu huku Bayer Leverkusen wakinyanyua taji lao la kwanza kabisa la Bundesliga.

Kimmich kwa sasa ana mkataba katika kikosi cha Vincent Kompany hadi 2025, na mustakabali wake wa muda mrefu bado haujaamuliwa. Bado anaweza kuhama msimu huu wa joto, baada ya hapo awali kuhusishwa na klabu za Arsenal, Manchester City, Barcelona na Real Madrid.

Akizungumza alipokuwa kwenye ziara ya kujiandaa na msimu mpya akiwa na Bayern, Kimmich alifichua kuwa 'milango iko wazi' kwa klabu zinazotaka saini yake msimu huu wa joto.

"Mnaweza kuongea kila wakati kwa njia inayofaa," alisema. "Milango yote iko wazi kwa kila mtu.

"Kwa ujumla, ninajisikia raha sana hapa. Watoto wangu wote walizaliwa hapa, tulijenga nyumba. Bila shaka, msimu uliopita haukuwa na mafanikio, sivyo mimi na Bayern tunataka sasa, nina njaa, nimejaa nguvu."

Kwa Kimmich, nafasi ya kubaki Bayern inaweza kuwa ya kuvutia, huku kocha mpya Kompany akitarajiwa kuleta hisia mpya kwa upande wa Ujerumani.

## Zirkzee aeleza atakavyocheza Man United

**MANCHESTER,** England

MCHEZAJI aliyesajiliwa na Manchester United majira ya joto Joshua Zirkzee amefichua jukumu ambalo angependa kucheza katika mfumo wa Kocha Erik ten Hag.

Mashetani Wekundu hao, walimtangaza Zirkzee kama uhamisho wao wa kwanza ulioingia chini ya udhibiti wa INEOS wa shughuli za soka pale Old Trafford mnamo Julai.

Nyota huyo wa zamani wa Bologna aliisaidia timu yake kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, na kusajili mechi 37 na mabao 12 katika kipindi chote cha kampeni. Anakaribia kuwa sehemu muhimu ya msimu ujao wa Ligi Kuu kwa United, akiungana na Rasmus Hojlund mbele ya safu ya ushambuliaji.

Nyota huyo wa Uholanzi anaamini kuwa, anaweza kutoa ujuzi 'tofauti' kuliko wachezaji wenzake na kueleza jukumu analotarajia kucheza katika pambano la mafanikio kwa United.

"Mara kwa mara mimi hushuka hadi katikati ya uwanja. Sifanyi hivyo kwa ajili yangu bali kusaidia timu," alisema akiiambia The Mirror.






# PSG yamtwaa Neves kutoka Benfica

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain imethibitisha kumsajili kiungo Joao Neves kutoka Benfica kwa ada ya euro milioni 70.

Neves mwenye umri wa miaka 19, alikuwa akihusishwa kwa kiasi kikubwa na kuondoka Benfica kwa kipindi kirefu cha mwaka huu, huku Manchester United mara nyingi wakitajwa kuwa wawaniaji wakuu.

Benfica walikuwa wamesisitiza mara kwa mara nia ya kupokea kipengele cha Neves cha kuachiliwa kwa jumla cha euro milioni 120 lakini wakakubali ofa ya euro milioni 70 kutoka kwa PSG, ambao walithibitisha kuwasili kwa kiungo huyo chipukizi Jumatatu.

"Ni fahari kubwa kwangu kujiunga na Paris Saint-Germain, klabu yenye malengo makubwa," alisema Neves baada ya kusaini mkataba wa miaka mitano.

"Nitatoa kila kitu kusaidia wachezaji wenzangu, kukua katika klabu hii nzuri na kushinda mataji mengi."

Mwenyekiti wa PSG, Nasser Al-Khelaifi aliongeza: "Tuna furaha kumkaribisha Joao Neves kuwa familia ya Paris Saint-Germain. Joao ni mmoja wa wachezaji wenye kipaji kikubwa nchini Ureno na duniani kote.

"Anajiunga na Paris Saint-Germain kwa ari kubwa na dhamira ya kupigania jezi yetu, ambayo ndiyo tunayotarajia kutoka kwa wachezaji wetu wote. Tunaendelea kujenga timu nzuri ya vijana huko Paris Saint-Germain - kulingana na kazi ya pamoja, vipaji na moyo wa pamoja ambayo ni msingi wa mustakabali mzuri wa klabu yetu."

Rais wa Benfica, Rui Costa hivi majuzi alikiri kusikitishwa kwake na kumpoteza Neves lakini akathibitisha kuwa ada ya ofa ilifanya washindwe kuwakatalia PSG.

"Ninaelewa ukosoaji wa mashabiki kwa sababu uchungu wao ni wangu," alisema Costa akiiambia A Bola.

"Lazima nitengeneze vikosi na kuhakikisha Benfica inaweza kutwaa mataji na unapompoteza mchezaji wa ubora wa Joao, ambaye alifunzwa hapa, najisikia huzuni zaidi. Ninamfahamu tangu akiwa na umri wa miaka 10 na ni vigumu kumuona akiondoka.

"Watu wanapaswa kuelewa kwamba tuliahirisha uhamisho huu kwa muda mrefu, tulikataa wazi mapendekezo ya kwanza, lakini tulifikia wakati fulani na namba ambazo zilifanya uhamisho kutoepukika."

Ingawa United huenda wakaikosa saini ya Neves, hatua hiyo bado inaweza kufanya kazi kwa faida yao kwani wanataka kumsajili kiungo mwingine, Manuel Ugarte, kutoka PSG.

Ripoti kutoka Ufaransa wiki iliyopita zilidai kuwa PSG itakuwa tayari kumtoa Ugarte kwa mkopo ikiwa watapata dili la Neves juu ya mstari huo.

# Homa ya dabi

INATOKA UKURASA 24

alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Cliford Ndimbo, amesema wanaendelea na maandalizi ya mwisho wa mchezo huo, akiwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi katika mchezo huo.

"Ngao ya Jamii ni mashindano ya kikanuni, kwa maana inaelekeza kuwa itazishirikisha timu nne ambazo zitacheza kwa mpangilio wa bingwa wa ligi kucheza na mshindi wa tatu na mshindi wa pili kucheza na wa nne, hii ni wiki ya moto, tutakwenda kucheza mechi nne, mbili za nusu fainali, fainali na kusaka mshindi wa tatu.

Kuna utofauti kati ya Ngao ya Jamii ya mwaka jana na hii, lilichezwa na timu nne, lakini ilikuwa kituo kimoja tu Uwanja wa Mkwakwani Tanga, lakini safari hii itachezwa katika vitu viwili, Zanzibar na Bara kwa mechi za nusu fainali, ila mshindi wa tatu na fainali, zote zitapigwa Benjamin Mkapa," alisema.

# ...Azim Dewji

INATOKA UKURASA 24

ya Jamii, kuashiria kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu.

Akizungumzia timu hizo mbili, Dewji alisema zote zina wachezaji wazuri kwa jinsi walivyoziona kwenye Simba Day na kilele cha Wiki ya Mwananchi, lakini Simba inahitaji muda ili wachezaji wake wazoeane zaidi kabla ya kuwa tishio.

"Yanga na Simba zina wachezaji wazuri, lakini Simba wanatakiwa kukaa na kuelewana kwanza, timu yoyote ili iwe nzuri ni lazima kwanza ikae pamoja wachezaji wazoeane.

Simba ina wachezaji 13 wote ni wapya kwenye kikosi, hivyo itawachukua muda mpaka kukaa vizuri, alibainisha.

Mwanamichezo huyo pia alionyesha kutoridhishwa na timu zote mbili kutokuwa na wachezaji wengi wa Kitanzania, tofauti na timu ya Red Arrows ya Zambia na APR ya Rwanda ambazo zilikuwa na wazawa wengi kuliko wageni.

"Haswa wale Wazambia, walikuwa na asilimia 90 wachezaji wa Kizambia, sijui wachezaji wetu wanakosea wapi?" alishangaa.

Hata hivyo akakumbuka kuwa huko nyuma michezo iliondolewa shuleni, ni hivi karibuni tu ndiyo imerudishwa.

"Mimi naona tulifanya makosa kuondoa mpira shuleni, kule ndiyo unaanza kuona kipaji cha mchezaji, siku hizi naona wamerudisha, sasa tuangalie miaka kadhaa ijayo," alisema Dewji.

# MASHUJAA, PAMBA, FOUNTAIN GATE KUFANYA MATAMASHA YAO J'MOSI

Na Adam Fungamwangwo

JUMAMOSI ijayo inaweza kupachikwa jina la 'Jumamosi ya Matamasha', ambapo jumla ya timu nne za Ligi Kuu Tanzania Bara zinatarajia kufanya matamasha yao kama ilivyokuwa kwa Simba Day na kilele cha Wiki ya Mwananchi.

Kama inavyoeleweka kuwa matamasha hayo ni maalum kwa ajili ya kutambulisha wachezaji, burudani na kucheza mechi ya kirafiki na mara nyingi zinakuwa ni timu kutoka nje ya nchi.

**Timu ya Mashujaa, yenyewe itakuwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, ambapo itakuwa na siku iliyopachikwa jina la 'Mashujaa Day' ambapo pamoja na burudani kadhaa, itamalizia tamasha hilo kwa kucheza dhidi ya Inter Star kutoka Burundi.**

Jijini Mwanza, timu ya Pamba ambayo imepanda daraja msimu huu, nayo itakuwa na siku yao walioipa jina la 'Pamba Day', ambapo baada ya burudani na kutambulisha wachezaji wake, itakipiga dhidi ya Vital'O ya Burundi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Pamba Day, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, amesema maandalizi yote ya tamasha hilo yamekamilika, hivyo kuwataka wakazi wa Mwanza na vitongoji vyake kujitokeza kwa wingi.

Pamba itacheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu huu baada ya miaka 23, kwani ilishuka daraja 2001.

Timu ya Fountain Gate yenyewe itafanya tamasha lake kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, mkoani Manyara, ambapo pamoja na shughuli zingine za kiburudani, litahitimishwa kwa kucheza dhidi ya Gor Mahia ya Kenya.

Singida Big Stars nayo siku hiyo hiyo, itacheza dhidi ya Agle Noir ya Burundi, Uwanja wa Liti, Singida, na matamasha yote hayo yanafanyika ikiwa zimesalia wiki moja tu kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuanza.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya wenye ulemavu, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *BMTZ kutoa mafunzo zaidi kwa watendaji wake*

Hawa Abdallah

BARAZA la Taifa la Michezo Zanzibar, BTMZ, limesema litaendelea kuhimiza viongozi wa vyama vya michezo kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji wao ili waweze kuwa na uhakika na ufahamu wa kitu ambacho wanakisimamia.

Hayo yalielezwa na Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Said Marine wakati wa ufungaji wa mafunzo ya wiki moja kwa Makocha na Waamuzi wa mchezo wa Netball visiwani hapa.

Alisema ni muhimu kwa viongozi kupata mafunzo ya mchezo unaosimamia ili kujijengea uweledi zaidi hasa katika kuhakikisha mchezo huo unasonga mbele.

Alisema mafunzo hayo ambayo yaliendana na kufundishwa sheria 21 za mchezo huo ambazo zimeongezeka mpya kutoka 13 ni jambo la busara litakalowafanya walimu hao kuingia katika ligi wakiwa na uwelewa wa kutosha juu ya sheria.

"Kupata mafunzo haya yatawasaidia kuendesha shughuli zenu kiufanisi zaidi, lakini kwa kiasi kikubwa kutapunguza migogoro ya maamuzi kwasababu nyote mnauwelewa wa mambo haya tena kitaaluma," alisema.

Naye Katibu wa chama hicho, Said Ali Mansab alisema mafunzo hayo yalilenga kuwafundisha walimu hao juu ya uwepo wa mabadiliko ya sheria za mchezo huo ili watakapoingia kwenye ligi waweze kuzitambua.

Alisema kuwa jumla ya washiriki awali walikuwa 30 lakini waliopatiwa vyeti ni 27 baada ya watatu kishindwa kuendelea kutokana na sababu tofauti.

Mwenyekiti wa chama hicho, Nasra Juma aliwataka walimu hao kujitahidi kutumia fursa za mafunzo zinazotolewa kila mara ili kukijengea uwelewa juu ya mambo mbalimbali yanayohusu mchezo huo.

Alifahamisha kwamba kupata mafunzo na kujitokeza kuusoma mchezo ni njia moja nzuri ya kuuendeleza mchezo huo na jitihada zao ndio ambazo zitawafanya wafike mbali.

Kwa upande wao washiriki wa mafunzo hayo Ashrak Bakar Juma kutoka timu ya Zimamoto alisema kupata mafunzo hayo ni chachu ya wao pamoja na wachezaji wao wanaowafundisha.

Hivyo alisema pamoja na kuwa sheria nane zimeongezeka na mpya kwao wao watakuwa mabalozi wazuri kwa wenzao pamoja na wachezaji wao kuwafahamisha ili waweze kuzielewa.

# Michezo

Jumatano Agosti 7, 2024

Nipashe



Zirkzee aeleza atakavyocheza Man Utd UKURASA 22



Gamondi

Fadlu

## ...Azim Dewji atia neno

**Na Adam Fungamwango**

MFADHILI Mkuu wa zamani wa Simba, Azim Dewji, amewatahadharisha wanachama na mashabiki wa timu za Simba na Yanga wasiende mpirani na matokeo mfukoni, kwani mechi za dabi siku zote hazina mwenyewe, kwani mara nyingi imetokea timu bora kupoteza mechi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Dewji, ambaye alifadhili Simba miaka ya 1990, na kuiwezesha kufanya vizuri kwenye michuano mbalimbali, ikiwamo kutwaa Ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la Kagame na kufika fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF, wakati huo likiitwa Kombe la CAF mwaka 1993, amesema kwa uzoefu wake katika masuala ya soka, hasa kwenye mechi za dabi kati ya Simba na Yanga matokeo yanaamuliwa na dakika 90 tu za mchezo, na wala si ubora wa kikosi kwa wakati husika.

Alisema ni kweli kuna wakati ubora huamua mechi hizo, lakini mara kwa mara imetokea Simba dhaifu kuifunga Yanga bora na Yanga ambayo haipo vizuri msimu huo kuifunga Simba iliyo kwenye kiwango cha juu.

"Dabi haina mwenyewe, matokeo yanategemea uwezo wa siku hiyo tu jinsi wachezaji watakavyopambana, timu gani wachezaji wale wameamka vizuri, au mbinu za walimu, huwezi kusema eti Simba watafungwa kesho kutwa, mechi za dabi hazitegemei hivyo, haiangaliwi timu gani bora," alisema Dewji ambaye alitamba akiwa Simba huku upande wa Yanga kukiwa na marehemu, Abbas Gulamali, aliyekuwa mfadhili wa Yanga na Mbunge wa Jimbo la Kilombero.

Simba na Yanga zinatarajiwa kukutana kesho, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, katika mechi ya Ngao

INAENDELEA UKURASA 23

# HOMA YA DABI SIMBA, YANGA NYUZI JOTO 90

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Makocha, wachezaji na wanachama wakoleza...

HOMA ya pambano la watani wa jadi, Simba na Yanga limeanza kuwapata wanachama na mashabiki wa timu zote mbili, ambapo pamoja na kila upande kutamba, lakini kumekuwa na angalizo kutokana na kile kilichoonekana kwenye mechi za matamasha yao.

**Timu hizo kubwa na kongwe zinazobeba taswira ya soka la Tanzania, zitavaana kesho saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam katika mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii.**

Wanachama na mashabiki wa Yanga wameendelea kutamba baada ya kuona kikosi chao kiko kwenye kiwango kile kile cha msimu uliopita, lakini kikiongezewa nguvu na wachezaji mastaa wanaolijua vyema soka la Bongo, Clatous Chama, Duke Abuya, Prince Dube na Jean Baleke, hivyo wamekuwa na uhakika kuwa wataendeleza ubabe wao kwa kuifunga Simba kama walivyofanya msimu uliopita, walipoifunga mara mbili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa upande wa wanachama na mashabiki wa Simba nao wameonekana kuwa na matumaini mapya, hasa baada ya kufanya usajili mkubwa wa wachezaji kutoka Ivory Coast, Zambia, Nigeria, Guinea, Burkina Faso na sehemu mbalimbali.

Wachezaji kama Joshua Mutale, Debora Fernandes Mavambo, Jean Charles Ahoua, Augustine Okejepha, Awesu Awesu, Valentin Nouma na wengineo wameanza kuwapa kiburi mashabiki wa Simba ambao wamesema wanaweza kupata ushindi, lakini hata kama watapoteza mechi hiyo, haitokuwa kizembe kama walivyochapwa mabao 5-1 msimu uliopita.

Wengi wameridhishwa na kiwango cha wachezaji wao, ingawa wanadai bado hawajazoeana na hicho pekee ndicho kinachowapa wasiwasi kwenye dabi hiyo, wengine wakisema baada ya mechi tatu tu za Ligi Kuu, hakuna timu inayoweza kuigusa tena, ikiwamo Yanga.

Kocha Mkuu wa Simba, Msauzi, Fadlu Davids, amesema hivi sasa anawaandaa wachezaji wake kisaikolojia kwa ajili ya mechi hiyo.

Alisema wachezaji wake ingawa mwenyewe anasema hawajaiva kwa asilimia 100 kama anavyotaka, na hii inatokana na muda kuwa mfupi kwani anaendelea kuwatengeneza, lakini wataifanya kazi kubwa keshokutwa.

"Mchezo utakuwa mzuri na mgumu, lakini nimewaandaa wachezaji wangu kisaikolojia kwenda kucheza, wakituliza akili na kufuata maelekezo, haina shaka ya kuibuka na ushindi," alisema.

Simba inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa ndiyo mshindi wa Ngao ya Jamii iliyopita ilipolitwaa Agosti 23, mwaka jana, Uwanja wa Mkwakwani, ilipoichapa Yanga mabao 3-1 kwa mikwaju ya penalti.

Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi amesema wanakwenda kucheza mchezo wa dabi ambao ndiyo utafungua msimu, akiahidi wachezaji wake kuwapa burudani mashabiki watakaofika uwanjani.

"Natumaini wachezaji wangu watacheza soka safi, na siku zote ukiwa bora na kucheza soka zuri, ushindi unakuwa upande wako,"

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002